# Nipashe

Alhamisi Februari 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580147

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Vigogo wengine 6 wahojiwa na Takukuru kashfa kina Lugola

UKURASA 3




UKURASA 13

# Sakata la Lissu laibuka upya



**KAMATI** ya kimataifa yataka kuchunguza shambulio la kupigwa risasi, mwenyewe afunguka mazito...

*Endelea ukurasa wa 2*



## CHINA YAMHAKIKISHIA JPM USALAMA WATANZANIA 400

UKURASA 2

Rais John Magufuli akiwa katika mazungumzo na Balozi wa China hapa nchini, Wang Ke, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Babu miaka 74 jela maisha kwa ubakaji

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** TFF YAWAKALIA MAREFA KITAKO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

## Benki ya Dunia yawaondoa hofu Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Dunia (WB) imesema uhusiano wake na Tanzania ni imara na kuihakikishia serikali ushirikiano madhubuti katika sekta mbalimbali za kimaendeleo.

Mkurugenzi Mkazi wa WB, Mara Marwick, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi.

Alisema Benki ya Dunia inathamini uhusiano huo wa tangu miaka ya 1960 hadi leo na iko tayari kuendelea kuunga mkono kwa njia ya ufadhili au mikopo ya miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

"Tuna uhusiano mzuri katika miradi na uwekezaji ambapo tunaiwezesha serikali katika maeneo mbalimbali. Pia tunafanya kazi pamoja katika masuala muhimu kama vile uchambuzi wa sera za maendeleo. Hii inaashiria kuwa Benki ya Dunia itaendeleza ushirikiano huu katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na uhusiano imara pamoja na maendeleo endelevu," alisema kama alivyokaririwa na taarifa ya wizara.

Taarifa hiyo ilisema mkurugenzi huyo na Waziri Kabudi walijadili masuala muhimu kuhusu maendeleo ya Tanzania hususani elimu, miundombinu, uchumi wa viwanda na maendeleo ya wananchi.

Kwa upande wake, Prof. Kabudi alisema Tanzania itaendeleza uhusiano na Benki ya Dunia na kuwataka Watanzania kupuuza uzushi na uvumi unaosambazwa katika mitandao ya kijamii na badala yake wasubiri taarifa rasmi kutoka kwa serikali na benki hiyo.

"Uhusiano kati ya Tanzania na Benki ya Dunia ni imara na unaendelea vizuri. Mkurugenzi wa Benki ya Dunia ametuhakikishia kwamba katika kipindi hiki ambacho yeye ni mkurugenzi, atauendeleza uhusiano huo.

"Mengi yanasemwa, lakini hayana ukweli na wakati mwingine si busara kwa kila yanayosemwa kuyajibu kwa sababu yanaweza kuwaondoa kwenye shughuli za msingi na mkajikuta kila siku mnajibu uvumi au uzushi katika mitandao ya kijamii na mambo mengine," alisema Prof. Kabudi. Aliongeza kuwa katika mazungumzo hayo pia wamegusia miradi ya kimkakati ambayo Tanzania inaitekeleza, mingine kwa fedha za ndani au kwa kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia.

"Tumezungumza kwa kirefu kuhusu mashirikiano katika elimu hasa elimu ya wasichana na kukuza rasilimali watu na kutaja maeneo mengine ya ushirikiano ambayo ni pamoja na sekta za miundombinu, afya, maji na nishati," ameongeza Prof. Kabudi.

Prof. Kabudi ameongeza kuwa Tanzania inakopesheka kwenye Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (EADB) na taasisi nyingi za kifedha.

Pia alisema serikali huhakikisha kuwa vigezo vyote vinavyotakiwa vinasimamiwa, lakini kikubwa hulipa madeni iliyokopa ndiyo maana inaaminiwa na kukopeshwa zaidi na fedha yote inayokopwa hupelekwa kwenye miradi ya msingi ya kulifanya taifa kujitegemea lenyewe katika miaka michache ijayo.

# Sakata la Lissu laibuka upya

**Na Enock Charles**

KAMATI ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), imependekeza wajumbe wake kumsindikiza kurejea nchini Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu.

Imeelezwa kuwa mapendekezo hayo yana lengo na kamati hiyo ipate fursa ya kukutana na mamlaka za kiserikali, kibunge na kimahakama na wadau wengine ili kuiwezesha kuelewa suala la kupigwa risasi kwa kiongozi huyo.

Katika taarifa yake jana, Lissu alidai kamati hiyo imetoa mapendekezo hayo ikiwa ni sehemu ya hatua inazozijua kufuatia malalamiko aliyoyawasilisha katika umoja huo.

"Kamati inatambua kwamba ninataka kurudi Tanzania haraka iwezekanavyo, na inapendekeza kuwa ujumbe wa kamati unisindikize wakati nitakaporudi, kwa imani kwamba kutembelea Tanzania kutatoa fursa ya kukutana na mamlaka za kiserikali, kibunge na kimahakama pamoja na wadau wengine, ili kuiwezesha kamati kuelewa suala hili vizuri zaidi," alisema.

Lissu aliwasilisha malalamiko IPU kwa kile anachodai kutotendewa haki na Bunge la Tanzania alipovuliwa ubunge, huku akiomba kufanyika uchunguzi wa tukio la kupigwa risasi Septemba 2017 mjini Dodoma, wakati akirejea nyumbani kwake baada ya kikao cha Bunge.

Mtaalamu huyo wa sheria, alivuliwa ubunge mwaka jana baada ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kudai ni utoro bungeni na kutokujaza kwa fomu za tamko la mali na madeni kwa miaka miwili mfululizo.

Katika taarifa yake ya jana, Lissu pia alidai IPU pia imeomba maelezo kutoka Bunge la Tanzania kuhusu sababu na hoja za uamuzi wa kuvuliwa ubunge na kuomba kutembelea Tanzania. Lissu pia alidai kuwa umoja huo umesikitishwa na jaribio la mauaji dhidi yake. Mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, aliahidi kuwasaidia wanasiasa wengine waliovuliwa ubunge, kuwasilisha malalamiko yao kwenye kamati ya umoja huo.

Alisema kamati hiyo imeshafanya uchunguzi na kutoa majibu kwa watu wengi waliokumbana na baa la kuvuliwa ubunge, akiitolea mfano Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo ina wabunge wake walionufaika na kamati hiyo.

"Ushauri wangu ni kwamba wabunge wetu wote ambao wameathiriwa na vitendo hivi, wawasilishe malalamiko yao kwa IPU ili yachunguzwe.

"Mtaona kwenye taarifa hii jinsi ambavyo malalamiko kutoka sehemu mbalimbali duniani, ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, yameshughulikiwa.

"Kama hili linakubalika, niko tayari kuwasaidia kuandaa hoja za kupeleka IPU au, bora zaidi, kuwaomba mawakili wangu wa London, yaani Amsterdam & Partners, kufanya hivyo kwa niaba yetu wote," ilisema.



Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, akisalimiana na Maofisa Uhamiaji baada ya kuwasili katika Makao Makuu ya Uhamiaji, jijini Dar es Salaam, jana, akiwa katika ziara maalum ya kujitambulisha kwa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, tangu aapishwe. Kushoto ni Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala. **PICHA: JESHI LA MAGEREZA**

# JPM ahakikishiwa usalama wa Watanzania 400 corona China

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli jana alikutana na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Tax, Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfred Fanti na Balozi wa China nchini, Wang Ke, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Baada ya kukutana na Balozi wa China, Rais Magufuli alimkabidhi barua aliyomwandikia Rais wa China Xi Jinping, akimpa pole kwa janga la homa ya virusi vya corona lililolikumba Jiji la Wuhan na kusababisha vifo vya mamia ya watu.

Mbali na kukabidhi barua hiyo, Rais Magufuli alisema Tanzania imeguswa na kulipuka kwa janga hilo na iko tayari kutoa ushirikiano wowote ambao Serikali ya China itahitaji katika jitihada za kukabiliana na homa hiyo.

"China ni ndugu zetu, ni marafiki zetu, tunatoa pole kwa Mheshimiwa Rais Xi Jinping na Wachina wote waliopatwa na madhara ya homa hii, daima Tanzania tupo pamoja na China na katika hili tupo pamoja pia," alisema.

Balozi Wang Ke alimshukuru Rais Magufuli kwa kuguswa na janga hilo na kuungana na China katika kipindi hiki kigumu.

Alitumia fursa hiyo kueleza hali ilivyo China, akibainisha kuwa Serikali ya China imeanza kupata mafanikio katika kukabiliana na homa hiyo.

Alisema imefanikiwa kuzuia isienee katika nchi zingine kwa ushirikiano na Shirika la Afya Duniani (WHO) na nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania.

Alimhakikishia Rais Magufuli kuwa licha ya Tanzania kutokuwa na mtu yeyote aliyethibitika kuambukizwa homa ya corona, pia Watanzania 400 walioko

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wakurugenzi na maofisa wa Mkoa wa Dar es Salaam, wakila kiapo wakati wa mafunzo ya Daftari la Kudumu la Mpigakura, jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vigogo wengine 6 wahojiwa Takukuru sakata kina Lugola

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewahoji 'vigogo' wengine sita waliohusika katika mkataba wenye utata wa ununuzi wa vifaa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mkataba huo ulioingiwa Agosti 22 mwaka jana kati ya jeshi hilo na Kampuni ya Rom Solution Co. Ltd, ndiyo uliosababisha kutumbuliwa kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na viongozi wengine wa wizara hiyo.

Jana, vigogo sita kutoka wizara hiyo walisalimisha kompyuta mpakato (laptop) katika Ofisi za Takukuru jijini Dodoma na kuhojiwa na taasisi hiyo kuhusiana na mkataba huo.

Waliohojiwa jana ni wajumbe wa kamati ya utekelezaji wa mkataba huo waliowasili Ofisi za Takukuru majira ya saa nne asubuhi.

Walioitwa na kufika katika ofisi hizo na kuhojiwa ni pamoja na Kamishna wa Fedha wa Jeshi la Zimamoto, Baraka Semwanza, Naibu Kamishna wa Zimamoto, Fikiri Salma, Naibu Kamishna wa Zimamoto Lusekelo Chaula, na Naibu Kamishna wa Zimamoto, Ully Mburuko.

Wengine ni Mchumi wa Jeshi la Zimamoto, Boniphace Kiponela na Mchumi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Felis Mshana.

Wiki iliyopita, Takukuru iliwahoji Lugola, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu, Naibu Waziri, Hamad Masauni na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ramadhan Kailima.

Vigogo hao wanahojiwa na taasisi hiyo nyeti kufuatia agizo la Rais John Magufuli la kutaka wahojiwe kutokana na kutia saini mkataba wa ununuzi wa vifaa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wenye thamani ya Euro milion 400 (zaidi ya Sh. trilioni moja).

# Kibabu chafungwa jela maisha ubakaji watoto

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida, imemhukumu kifungo cha maisha Daudi Karata (74), baada ya kumtia hatiani kwa makosa 13 ya kuwabaka wanafunzi.

Karata, maarufu kama Babu Seya (74), mkazi wa Mtaa wa Unyankindi, Manispaa ya Singida, amehukumiwa kifungo hicho baada ya kuthibitika pasi na chembe ya shaka kuwa aliwabaka wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi wenye umri kati ya miaka saba na 12.

Katika shauri hilo lililofunguliwa mahakamani hapo Oktoba 30, 2017 na kuanza kusikilizwa na Hakimu Mkazi Flora Ndale na baadaye kuendelea kusikilizwa na Hakimu Aristeda Tarimo hadi lilipotolewa hukumu, upande wa Jamhuri ulipeleka mashahidi 41 na vielelezo 24 kuthibitisha makosa dhidi ya mshtakiwa huyo.

Akitoa hukumu huiyo juzi, Hakimu Tarimo alisema katika shtaka la kwanza, la pili, la tano, saba, nane, 10 na 13, mahakama inamhukumu mshtakiwa kifungo cha miaka 30 jela na katika shtaka la nne, 11 na 12, inamhukumu kifungo cha jela maisha.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Patricia Mkina, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Karata alitenda kosa hilo tarehe isiyojulikana Oktoba, 2017 maeneo ya Mitunduruni Manispaa ya Singida kwa kumwingilia kimwili bila ridhaa mwanafunzi wa darasa la pili (jina lake na shule vinahifadhiwa).

Pia Mkina alidai kuwa kati ya Oktoba, 2016 na Oktoba, 2017, mshtakiwa alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi wa darasa la tano mwenye umri wa miaka 12 na katika shtaka la tatu, tarehe na mwezi usiojulikana, alimwingilia mwanafunzi mwenye umri wa miaka 10 pia bila ridhaa yake.

Aliendelea kudai kuwa katika shtaka la nne, Agosti 2017 mshtakiwa alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi mwenye umri wa miaka tisa na Oktoba, 2017 akamwingilia tena mwanafunzi mwenye umri wa miaka 10.

Katika shtaka la sita, Mkina alidai kuwa kati ya Desemba 2016 na Oktoba, 2017 mshtakiwa akiwa maeneo ya Mitunduruni, alimwingilia bila ridhaa yake mwanafunzi mwenye umri wa miaka minane.

Pia alidai kuwa katika maeneo hayo hayo, kati ya Septemba, 2017 na OKtoba, 2017 Karata alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi mwingine mwenye umri wa miaka 10.

Katika shtaka la nane, ilidaiwa kwamba mwaka 2017 Karata akiwa maeneo ya Mitunduruni alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi mwenye umri wa miaka tisa na Oktoba 16, 2017 saa 7:50 mchana, akiwa Mitunduruni, alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi mwingine mwenye umri wa miaka 10.

Aidha, Mkina aliendelea kudai kwamba Oktoba, 2017 mshtakiwa huyo akiwa Mitunduruni, alimwingilia bila ridhaa mtoto wa miaka tisa na mwaka huo huo, tarehe isiyojulikana, alimwingilia mtoto wa darasa la kwanza (shule inahifadhiwa).

Kadhalika mwendesha mashtaka huyo wa serikali alidai kuwa mwaka 2016 hadi Oktoba, 2017 Karata akiwa Mitunduruni alimwingilia bila ridhaa mwanafunzi mwenye umri wa miaka saba. Hata hivyo, mshtakiwa alikana kutenda mambo hayo baada ya kusomewa mashtaka yaliyokuwa yakimkabili.

# Ajiua gesti kisa msongo wa mawazo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ALIYEKUWA Meneja wa Chama cha Ushirika wa Wakulima Ngara, Humphrey Kachecheba (50), anadaiwa kujiua katika nyumba ya kulala wageni kwa kile kinachodaiwa ni msongo wa mawazo kutokana na kukabiliwa na upotevu wa fedha Sh. milioni 889 mali ya chama hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema jana kuwa mtu huyo aligundulika Februari 3, mwaka huu, saa 3:00 usiku akiwa chumba namba saba katika nyumba ya kulala wageni ya New Praise Lodge iliyoko Hamugembe, Manispaa ya Bukoba.

"Uchunguzi wa awali wa polisi, umebaini kuwa Kachecheba ambaye alikuwa mkazi wa Bunazi wilayani Missenyi, alichukua chumba katika nyumba hiyo ya wageni tangu Januari 29, mwaka huu, saa 4:00 asubuhi akitokea Wilaya ya Ngara alikokuwa akifanyia kazi na aliendelea kuishi hapo hadi alipogundulika akiwa amefariki dunia," alisema.

Malimi alisema kutokana na maelezo ya wahudumu, muda wote alikuwa anashinda ndani ya chumba kutwa nzima na kutoka usiku majira ya saa 2:00 na kurejea saa 4:00 usiku.

"Mwili wa Kachecheba uligunduliwa na mhudumu na nyumba hiyo ya wageni aitwaye Odetha Edmund, alipotaka kufanya usafi ndani ya chumba hicho baada ya kugonga mlango bila kupata majibu, huku ukiwa umefungwa kwa ndani," alisema.

Kwa mujibu wa Malimi, mhudumu huyo alilazimika kusubiri hadi saa 10:00 jioni na kurudi kumgongea tena, lakini bado Kachecheba hakufungua na ndipo alipotoa taarifa kwa meneja wake ambaye naye alitoa taarifa polisi.

INAENDELEA UK. 8

# Bunge lataka mkataba mgodi madini uvunjwe

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuuvunja mkataba wa uendelezaji wa Mgodi wa Buckreef kati ya Kampuni ya Tanzam 2000 na Shirika la Madini la Taifa (Stamico) kutokana na kugubikwa na masharti hasi.

Wakati Bunge likitaka kuvunjwa kwa mkataba huo, imedaiwa tayari mbia mwenza amevunja masharti mengi ikiwa ni kufanya ununuzi wa mtambo bila Stamico kushirikishwa.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu na shughuli za kamati kwa mwaka 2019/20, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula, alisema serikali kama wataona inafaa, ni vyema wakavunja mkataba huo kwa kushindwa kuendeleza mgodi huo hadi sasa.

Alisema kamati hiyo inatoa rai kwa serikali kuwa ni vyema mkataba huo ukasitishwa kwa kuwa ni dhahiri kuwa hauna manufaa na kuna ukiukwaji mkubwa wa makubaliano ya kimkataba, hivyo taifa linapoteza mapato ambayo yangetokana na uendelezaji wa mgodi.

"Serikali kama wataona inafaa ni vyema wakavunja mkataba na Kampuni ya Tanzam 2000 katika kuendeleza Mgodi wa Buckreef kwani masharti hasi yako mengi na mbia mwenza amevunja masharti mengi, mfano ununuzi wa mtambo bila Stamico kushirikishwa pamoja na kutokuendeleza mgodi hadi sasa.

"Ni rai ya kamati kuwa katika maeneo ambayo Stamico inashindwa kuendeleza uzalishaji ni afadhali maeneo hayo yakagawiwa kwa wachimbaji wadogo ili serikali iendelee kukusanya mapato," alishauri.

Alisema katika kuendeleza mradi wa ubia wa dhahabu wa Buckreef, Stamico iliingia mkataba wa ubia na Kampuni binafsi ya Tanzam 2000 ambayo ni kampuni tanzu ya Tanzanian Royalty Exploration Corporation (TRX) ya Canada Oktoba 2011.

Kwa mujibu wa kamati hiyo, katika mkataba huo, Stamico inamiliki asilimia 45 ya hisa na Tanzam 2000 wanamiliki asilimia 55.

Ubia huo unahusisha leseni maalum ya uchimbaji mkubwa (special mining license) Na. SML 04/92 na leseni 13 za utafutaji wa madini.

Mpaka sasa mradi huo unatajwa kuwa na vikwazo vingi hususani vya kuchelewa kuanza kwa uzalishaji, jambo ambalo linasababisha shirika kukosa mapato.

Bunge limearifiwa kuwa tayari Tume ya Madini imemwandikia mbia huyo ambaye ni Kampuni ya Tanzam 2000 hati ya makosa (default note), ikiwa ni jitihada ya kuangalia upya namna bora ya kuendeleza mradi huu kwa manufaa ya taifa.

# Sheria usalama barabarani kufumuliwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KIBANO dhidi ya madereva wa vyombo vya moto wanaosababisha ajali kisha kuchukulia poa kesi zinazopelekwa mahakamani sasa kinanukia, baada ya Bunge kuagiza Jeshi la Polisi kuharakisha mchakato wa kuifumua sheria ya usalama barabarani ili kuundwa upya.

Jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Salum Mwinyi Rehani, alisema wakati Jeshi la Polisi linaendelea na mchakato wa kupeleka muswada huo bungeni, ni vyema elimu kwa umma iendelee kutolewa hasa kwa madereva wa pikipiki, maarufu kama bodaboda.

Rehani alikuwa akiwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

"Kucheleweshwa kwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani kunaendelea kusababisha majeruhi na vifo kutokana na kukosekana kwa Sheria ya Usalama Barabarani iliyojitosheleza katika nyanja zote. Na kwa kuwa bado kuna umuhimu wa kupunguza kabisa ajali zinazosababishwa na makosa ya barabarani, Jeshi la Polisi liharakishe kuleta marekebisho ya sheria hiyo," alisema mwenyekiti huyo

Aidha, taarifa ya kamati hiyo, imeeleza kuwa makosa ya usalama barabarani yameendelea kusababisha ajali ambazo wakati mwingine husababisha mauti na hata ulemavu wa kudumu.

Alisema ni lazima sheria hiyo ifumuliwe, kwa kuwa serikali imeonyesha nia ya dhati ya kupunguza makosa ya usalama barabarani, ambapo makosa hayo yamepungua kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na mwaka 2018.

**MSONGAMANO MAHABUSI**

Kuhusu msongamano wa mahabusi na wafungwa magerezani, alisema katika kipindi cha Agosti, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu suala hilo.

Alisema kamati ilielezwa kuwa idadi ya wahalifu magerezani hubadilika kati ya 36,000 na 39,000 ilhali uwezo wa magereza ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kwa siku.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa, hadi Juni 30, mwaka jana, idadi ya wahalifu ilikuwa 37,574 na kati ya hao, mahabusi walikuwa 18,729.

Alisema kwa takwimu hizo zilizotolewa ni dhahiri kuwa ipo changamoto ya mahabusi wengi kukaa magerezani bila kesi zao kushughulikiwa na kumalizwa kwa muda mfupi.

Alieleza kuwa kamati hiyo ilitaka kujua kuhusu hali inayosababisha msongamano wa mahabusi magerezani licha ya kuwa kamati imekuwa ikiishauri mara kwa mara serikali kuhusu hatua za kuchukua ili kupunguza msongamano huo.

Alifafanua kuwa kamati ilibaini kuwa, masuala ambayo yameendelea kuchangia msongamano huo ni kutokana na magereza mengi yaliyopo kujengwa muda mrefu uliopita kwa mahitaji ya huduma hiyo kwa wakati huo wa ukoloni.

Alisema kuwa licha ya idadi ya watu na uhalifu kuongezeka, hakuna nafasi zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya kuhifadhi wahalifu Magereza mengi ni chakavu kiasi cha baadhi ya mabweni ya wahalifu kutotumika tena hivyo kupunguza zaidi nafasi za kuhifadhi mahabusi.

Nyingine ni ukosefu wa magereza ya wilaya katika wilaya nyingi zilizopo na zilizoanzishwa umesababisha msongamano wa mahabusu katika maeneo ambayo inabidi kuhifadhi mahabusi wa wilaya nyingine katika wilaya husika ambapo kwa sasa zisizo na magereza ni 52. Ucheleweshaji wa kesi mahakamani ambao husababisha mahabusi kukaa magerezani kwa muda mrefu kabla ya mashauri yao kumalizika, alisema ni ongezeko kubwa la wahamiaji haramu wanaoingia nchini kinyume cha sheria na kupelekwa magerezani.

Pia alisema Jeshi la Magereza linakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji yakiwamo magari ya kusafirisha mahabusi kwenda na kurudi mahakamani.

Sambamba na hilo, alisema serikali ihakikishe upelelezi wa kesi hususan zile ambazo si za jinai, hauchukui muda mrefu, iendelee kutumia utaratibu wa mahakama inayotembea ili kushughulikia kesi nyingi zaidi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kusitisha kwa huduma za usafiri wa treni za abiria na mizigo kwa njia ya reli ya kati. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mvua yakwamisha tena usafiri wa reli

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Reli (TRC), limesitisha huduma za usafiri wa treni za abiria na mizigo kwa njia ya reli ya kati kutokana na uharibifu uliosababishwa na mafuriko katika maeneo ya Kilosa, Igandu, Dodoma na Makutupora kufuatia mvua inayoendelea kunyesha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TRC, Jamila Mbarouk, mvua hiyo imesababisha kufurika kwa mito mikubwa.

"Takriban maeneo 26 yameathirika, na kati ya hayo, 10 yako katika hali mbaya, tuta la reli na baadhi ya makaravati yamezolewa na maji.

"TRC inaomba radhi kwa wadau wa sekta ya miundombinu ya reli kusimamisha huduma za uchukuzi kwa abiria na mizigo hasa kati ya Dar es Salaam na Dodoma mpaka hapo hali itakapotengamaa, ikizingatiwa mvua bado inaendelea kunyesha," alisema.

Mbarouk alisema tayari wahandishi wa shirika hilo wako katika maeneo mbalimbali yaliyoharibika kwa ajili ya kufanya tathmini halisi ya gharama za miundombinu ya reli iliyoathirika.

"Matengenezo ya muda mfupi yanaendelea katika maeneo ambayo maji yamepungua ili kurejesha huduma za usafiri wa treli za abiria na mizigo na hadi sasa maeneo ya kati ya Dodoma na Makutupora yamerekebishwa," alisema.

HABARI KITAIFA




Mwenyekiti wa vyama visivyo na wabunge ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha DP, Abdul Mluya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kupinga vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wabunge wa upinzani vya kuzuia mikopo kutoka Benki ya Dunia. Kulia ni Katibu Mkuu wa chama cha NRA, Hassan Almas. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mpango azipa neno nchi SADC mwenendo uchumi

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema nchi za Afrika hasa zilizopo chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), zinatakiwa kujitazama na kushauriana kuhusu mwenendo wao wa uchumi badala ya kuyaachia mashirika ya kimataifa pekee.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dodoma wakati wa mkutano kati yake na ujumbe wa SADC unaoongozwa na Sikumbuzo Dlamini, ambao umetembelea nchini kwa ajili ya mpango wa kujitathmini kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Dk. Mpango alisema nchi za Afrika zimezoea kuona Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kuja kuangalia namna uchumi unavyoendelea ilhali Afrika hasa nchi za SADC zina fursa pia ya kutembeleana na kushauriana namna bora ya kuendeleza uchumi na kuwahudumia wananchi, ikizingatiwa zinafahamiana vizuri.

"Madhumuni ya ujumbe wa SADC kutembelea nchini ni kuangalia hali ya ukuaji wa uchumi, ubadilishanaji wa fedha za kigeni, mauzo ya bidhaa ndani na nje ya nchi na kushauri mahali ambapo Tanzania haijafanya vizuri au kutumia fursa ipasavyo," alisema.

Waziri huyo alisema nchi za SADC zilikubaliana kuchagua ujumbe ambao utakuja nchini kufuatilia namna uchumi mkuu unavyoendelea, hivyo akatumia fursa hiyo kueleza utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya umeme wa maporomoko ya Mto Rufiji, ujenzi wa reli ya kisasa na miundombinu ya barabara.

Kiongozi wa Ujumbe wa SADC, Sikumbuzo Dlamini, ambaye ni Meneja wa Sera za Uchumi na Takwimu wa Benki Kuu ya Eswatini, aliipongeza Tanzania kwa maendeleo makubwa iliyofikia baada ya kujionea miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya reli na miradi ya maji ambayo itasaidia ukuaji wa uchumi mkubwa na kuiwezesha kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

# ACT wajipanga kukimbilia kortini kuzuiwa muswada

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinakusudia kwenda mahakamani kupinga kinachokiita njama za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwasilisha hoja binafsi katika Baraza la Wawakilishi kuitaka serikali ipeleke muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho zilizoko Vuga mjini Zanzibar, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ya chama hicho, Omar Said Shabani, alidai taarifa ambazo wamezipata kutoka vyanzo vya kuaminika ndani ya CCM ni kwamba wapinzani wao hao wa kisiasa wamepanga kupeleka hoja binafsi Baraza la Wawakilishi kuitaka serikali ipeleke muswada huo.

Alidai mabadiliko yanayolengwa zaidi ni katika vifungu vya 43, 44 na 45 vya sheria hiyo na kuongeza kigezo cha kuwa mwanachama wa chama kinachomdhamini, anatakiwa awe mwanachama wa chama husika walau kwa miaka miwili kama sifa ya kugombea urais, ubunge, uwakilishi na udiwani.

"Taarifa zetu zinaeleza kuwa CCM wamekubaliana kuwa... (alitaja jina la mmoja wa wawakilishi) ndiyo awe mwasilishaji wa hoja hiyo kwenye moja ya vikao vya Baraza la Wawakilishi lilioanza kikao chake leo (jana)," alidai.

Aliendelea kudai kuwa hoja hiyo inaandaliwa kwa lengo la kupata dawa ya kuwazuia baadhi ya wanachama wapya wa ACT-Wazalendo kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Shaban alimtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar asishawishike na hoja hiyo, akidai kuwa ni mtego na ataingia katika rekodi mbaya.

# Manispaa yatakiwa ajira kukusanya taka

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imeitaka Manispaa ya Moshi, kuibua ajira mpya kwa vijana kwa kuwapa fursa ya kukusanya taka majumbani kibiashara na kupeleka katika eneo maalumu litakalotengwa badala ya mfumo unaotumika sasa.

Kwa sasa Manispaa inapitisha gari mitaani kubeba taka jambo linaloweza kufanywa na vijana hao na kupeleka katika kituo maalum ambacho kitatumiwa na Manispaa kubeba kwa pamoja na kupeleka dampo kuu.

Katibu tawala msaidizi, utawala na rasilimali watu mkoani humo, Bwai Biseko, alitoa rai hiyo wakati akifungua kikao cha mazingira kilichojumuisha viongozi wa mitaa na kata zinazozunguka msitu wa Rau ili kuondoa tatizo la utupaji taka msitu huo.

"Vijana wanaweza kutumika baada ya jamii kuchangia kiasi fulani cha fedha ili taka zirundikwe eneo moja, huku magari ya manispaa yakipita kukusanya katika vituo vikuu na hili linawezekana kama jamii itakua na dhamira ya dhati katika kubadilika katika usafi wa mazingira," alisema.

Alisema lengo la mipango hiyo ni kuhakikisha Msitu wa Rau unatumika kama sehemu ya utalii, lakini kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoleta athari za uharibifu wa mazingira.

Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Jomba Koyi, alisema Manispaa ina mipango ya kugeuza taka kuwa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa gesi.

"Tayari tumetangaza zabuni ya ujenzi wa dampo jipya eneo la Mtakuja nje ya Manispaa, na hadi kufikia Desemba mwaka huu taka zitakuwa mali na wananchi watauza taka zao badala ya kuzitupa...hii itabadili mtazamo na itatunza mazingira," alisema.

Ofisa Maliasili mkoani hapa, Emanuel Kiengi, alisema kikao hicho kilichoendeshwa kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) kimelenga kuhakikisha sheria, taratibu na mamlaka zinazosimamia misitu vinaheshimika.

Alitaka viongozi hao kubeba dhamana ya kulinda rasilimali za msitu huo kwa kutoa elimu kwa jamii inayouzunguka ili kuuhifadhi.

Awali, Ofisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Joshua Mungure, alithibitisha kuwapo kwa uchafu wa taka ngumu na nyinginezo katika msitu wa Rau, jambo ambalo halikubaliki na kutaka jamii kubadili tabia.

"Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002 inahusu sana misitu haswa ya asili katika sehemu ya tano kifungu 26 kinaeleza utunzwaji wa misitu iliyohifadhiwa kisheria imetaja masuala kama kuingia msituni kuangusha miti, kuchimba madini, mifugo watakaokwenda kinyume na hayo wakitiwa hatiani watalipa faini siyo chini ya Sh. milioni moja," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendelee kuchukua hatua dhidi ya mvua

**MVUA** zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini, zimeendelea kusababisha athari kwa wakazi wa maeneo husika.

Mvua hizo zilizoanza Septemba mwaka jana, zimekuwa zikiharibu miundombinu ya barabara na madaraja pamoja na majengo, vifo na kuwakosesha watu makazi kutokana na maji kuzingira nyumba na kuzibomoa.

Mvua ni neema na zinahitajika, lakini pale zinaponyesha na kusababisha madhara kwa binadamu inakuwa kinyume cha matarajio yake, kwa sababu matarajio ni kusaidia shughuli za uzalishaji wa chakula na mahitaji mengine ya maji yakiwamo matumizi ya nyumbani na katika taasisi.

Hatutataja matukio yote yaliyosababishwa na athari za mvua hizo, lakini matukio ya karibuni ni mvua kubwa ya mafuriko wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro, ambayo ilisababisha maelefu ya watu kupoteza makazi, hivyo kwenda kuishi kwa ndugu, jamaa, majirani na marafiki. Mvua hiyo pia ilisomba makaburi takribani 14.

Wakazi kadhaa wa Wilaya ya Mvomero waliopoteza makazi wanaendelea kujihifadhi kwa ndugu, jamaa, marafiki na majirani, huku wakiomba kupatiwa makazi ya muda pamoja na misaada ya kibinadamu kutoka serikalini, wadau na wasamaria wema. Katika tukio lingine, zaidi ya watu 1,000 wameripotiwa kukosa makazi, baada ya nyumba 237 kubomolewa na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Dodoma.

Wiki iliyopita watu zaidi ya 20 walifariki dunia mkoani Lindi kutokana na mvua kubwa zilizoambatana na mafuriko sambamba na kuwakosesha makazi mamia ya maelfu ya wananchi.

Mafuriko hayo yaliyozingira makazi mengi, yalisababisha wakazi wake kuokolewa kwa kuondolewa kwa msaada wa serikali. Kimsingi, athari za mvua zinazoendelea kunyesha zinaweza kuwa kubwa kama wananchi hawatachukua hatua kama mamlaka husika husan Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zinavyosisitiza wananchi kuchukua hatua.

Mamlaka hiyo imeshatabiri kuwa mvua zitaendelea kunyesha hadi Aprili, hivyo kutoa angalizo kwa wananchi kuchukua tahadhari, hivyo kwa upande wetu tunapenda kusisitiza wananchi wasipuuze kuchukua tahadhari.

Mvua zinazoendelea kunyesha sasa zinaweza kuunganisha na za masika, kwa hiyo wananchi wasiache kuendelea kuchukua hahadhari.

Tahadhari kwa watu wanaoishi maeneo hatarishi kama ya mabondeni na mapitio yote ya maji waondoke kwa kuwa kuwa uwezekano mkubwa wa kupata madhara yatokanayo na mafuriko. Ikumbukwe kuwa moja ya athari za mabadiliko ya tabianchi ni mvua ambazo hazifuati msimu, na zinaponyesha zinakuwa na athari nyingi ikiwamo mafuriko na upepo. Madhara yake yamezikumba nchi nyingi za ukanda wa Afrika Mashariki.


Athari hizi za mabadiliko ya tabianchi zinayakumba na kuyaathiri maeneo mengi duniani, hivyo Tanzania hatuwezi kuwa kisiwa badala yake tuchukue tahadhari.

Tukumbuke kuwa serikali haina uwezo wa kuwasaidia watu wote wanaopata athari ya mvua husan wale ambao wamekuwa wakikaidi maelekezo ya kuyahama maeneo hatarishi kwa muda mrefu.

Ni matumaini yetu kuwa wananchi wataendelea kuchukua hatua zote za tahadhari kutokana na taarifa pamoja na ushauri unaotolewa mara kwa mara na mamlaka husika.

Kadhalika, tunawashauri wananchi kuzitumia vizuri mvua hizi kwa ajili ya kilimo, kwa kuwa kwa kusubiri mvua za masika kunaweza kuwaathiri kama zitakatika kabla ya msimu rasmi wa kilimo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Wauguzi wenye tabia hii ni mzigo sekta ya afya

Na Sabato Kasika

**NENO** afya linatasfiriwa kama hali ya kujisikia vizuri kimwili, kiakili, kiroho na kiutu, bila ya kusumbuliwa na ugonjwa wowote.

Pia, afya hiyo hiyo ya binadamu, inaweza kuwa nzuri kama mhusika atafuatilia kanuni na taratibu bora katika kulinda mwili wake.

Ukienda kwenye tafsiri ya Shirika la Afya Duniani (WHO), lenyewe linafafanua kwa hatua zaidi, kwamba ni hali ya ustawi kamili kimwili, kiroho na kijamii na zaidi ya kukosa ugonjwa.

Kimsingi, afya bora ni rasilimali muhimu kibiandamu. Ndiyo maana, serikali inafanya kila njia kuhakikisha afya za watu wake inatunzwa. Hapo imajumuisha kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya katika kila kata, yote ni kusogeza huduma karibu na waliko watu.

Tunaenda mbali kwa kuhitaji kila wilaya kuwa na hospitali yake, lengo ni mkoa kuwa na Hospitali ya Rufani hadi ngazi ya kanda. Ukidodosa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), kinacholengwa ni kuhakikisha afya ya Watanzania zinakuwa bora kwa kupata matibabu yanayostahili, mahali aliko.

Uwepo wa zahanati, vituo vya afya na hospitali unakenda sambamba na kuajiri watumishi wa sekta hiyo, ambao ni muhimu kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wakiwamo wajawazito wanaoenda kujifungua.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo za serikali za kuboresha afya za Watanzania, kunakuwapo na malalamiko ya muda mrefu kwamba wapo baadhi ya wauguzi na wakunga wanaonyanyasa wajawazito.

Hiyo ni moja ya changamoto, inayowakumba baadhi ya kinamama wanaoenda katika vituo vya afya au hospitali kwa ajili ya kujifungua na kukutana na manyanyaso toka kwa baadhi ya wauguzi na wakunga.

Wanaorushiwa lawama zaidi ni wauguzi wakunga, wanaodaiwa hawahudumii ipasavyo, kwa mujibu wa majukumu yao, tena wengi wao ni wanawake wenzao na hata wanawasababishia usumbufu usio wa lazima, wahitaji hao wa huduma ya kiafya wanapotekeleza majukumu yao.

Manyanyaso hayo, yalishawahi kufikishwa bungeni kukihojiwa hatua gani ambazo serikali imechukuwa kuwadhibiti watumishi wa aina, ili wajawazito wasiendelee kunyanyaswa.

Katika sakata hilo la manyanyaso, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustin Ndugulile, alikiri lawama hizo kutoka kwa watumishi wake na kwamba wamekuwa wanyanyasaji wanawake, wanaoenda kujifungua bora na wizara husika inaendelea kuwafuatilia wanaolalamikiwa.

Sote tukubaliane, wauguzi na wakunga wenye tabia ya aina hiyo kwamba ni mzigo kwenye sekta ya afya, wanatakiwa kuzingatia maadili ya kazi na kuwa fani yao ni ya wito.

Mjamzito anapoenda katika kituo cha afya au hospitali kwa ajili ya kujifungua, anahitaji ahudumiwe na kurejea nyumbani salama, lakini anapokutana na matusi au kukosa huduma, hilo ni tatizo.

Serikali inaboresha huduma ya afya, na matarajio ya Watanzania kuipata bila manyanyaso wala aina yoyote ya vikwazo vinavyoweza kusababisha wajikute katika mazingira magumu.

Hivyo, litakuwa jambo la maana iwapo malalamiko dhidi ya baadhi ya wauguzi na wakunga yataisha ili kwenye maeneo yao ya kazi pale mahali salama la kupata huduma nzuri ya afya.

Mabadiliko ya tabia kwa wauguzi na wakunga wanaolalamikiwa, yatakuwa chachu ya huduma bora ya afya, kwani ni aibu na hatari kusikia mjamzito amepoteza mtoto kwa sababu ya uzembe wao.

Kwa mfano, katika ziara ambayo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewahi kuifanya mkoani Arusha, yapo mambo kadhaa yalijitokeza na hasa kwenye upande wa afya yakiwa malalamiko ya mazito.

Alielezwa magumu hayo ya kiutendaji na kuchelewa kupatikana matibabu. Ni simulizi nzito isiyofaaa, ina huzuni na ukakasi kurudiwa.

Kama kweli hilo lilitokea, ni wazi kwamba hayo unyanyasaji ambao wauguzi na wakunga wanatakiwa kuacha mara moja katika zama zilizopo, ni wazi huo ni mzigo mkubwa kwenye sekta ya afya na hatari kwa maisha ya Watanzania.

Wenye mtindo huo, watambue kuwa afya bora ni rasilimali muhimu, na inapaswa kulindwa, kuliko kuona kama jambo la kawaida kumwacha mgonjwa akihangaika kana kwamba hana haki ya kuishi.

HABARI KITAIFA

## SBL kufadhili wanafunzi 30

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 30 kutoka katika jamii za wakulima nchini, wamepatiwa ufadhili wa masomo kupata elimu ya kilimo katika vyuo vinavyofundisha masomo ya kilimo.

Ufadhili huo umetolewa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) katika mpango wake wa ufadhili wa masomo unajulikana kama Kilimo-Viwanda Scholarship, unaolenga kuongeza wataalamu wa kilimo watakaowasaidia wakulima nchini kuongeza uzalishaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mpango huo katika Chuo cha Kaole Wazazi cha Kilimo kilichoko Bagamoyo mkoani Pwani.

"Ni muhimu kwetu sisi kama SBL kuiunga mkono serikali katika kuwajengea uwezo wakulima wetu kupitia kuwaongezea wataalamu wa kilimo watakaosaidia kuwashauri na hivyo kuongeza tija katika kilimo," alisema.

Aliongeza kuwa Chuo cha Kaole Wazazi ni moja kati ya vyuo vitatu ambavyo kampuni ya SBL inashirikiana navyo katika kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo nchini.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mpango huo unawalenga siyo tu wanafunzi wanaotoka katika familia zenye vipato duni, bali pia wanafunzi wanaotoka katika jamii za wakulima katika sehemu mbalimbali nchini.

Alisema kila chuo kitapata nafasi ya kutoa wanafunzi 10 kila mwaka na watakaolipiwa ada na SBL mpaka watakapomaliza masomo yao.

Ocitti alisema mpango huo ni sehemu ya mkakati wa SBL wa kuongeza kiasi cha nafaka ambacho kampuni hiyo inanunua kwa ajili ya uzalishaji wa bia ambazo ni pamoja na mahindi, shayiri na mtama.

"Kampuni ya SBL ina lengo la kuongeza kiasi cha malighafi inayonunua kutoka kwa wakulima wa ndani hadi asilimia 85 kufikia mwaka 2020 na ndiyo maana tumeona umuhimu wa kusaidia kusomesha wataalamu wa kilimo ili wakafanye kazi ya kuboresha kilimo chetu. Kwa sasa kampuni inanunua malighafi kutoka kwenye mtandao wenye wakulima 400 nchini," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Kaole Wazazi College of Agriculture, Sinani Simba, aliishukuru SBL kwa kuja na wazo la kutoa ufadhili wa masomo ya kilimo na kuongeza kuwa ili kilimo kiwe cha tija wataalamu wengi wanahitajika.

"Tunayo furaha kwa kuwa ufadhili huu unawalenga wanafunzi wanaotokea katika familia zenye vipato duni ambao kama siyo msaada wa SBL, wasingeweza kupata fursa ya kuendelea na masomo," alisema.

# Vyama 12 vyapinga harakati kudai tume huru ya uchaguzi

**Na Mary Geofrey**

VYAMA 12 vya upinzani nchini, ambavyo havina wawakilishi bungeni, vimesema vimeshajiandaa kushiriki uchaguzi mkuu chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Viongozi wa vyama hivyo 12 wanapingana na harakati zinazoendelea nchini za baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani vyenye wawakilishi bungeni; ACT-Wazalendo, CUF), Chadema na NCCR-Mageuzi, vilivyodai tume huru ya uchaguzi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Democratic Party (DP), Abdul Mluya, alitoa msimamo huo kwa niaba ya viongozi wenzake walipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana. Alidai upinzani wote nchini unahitaji kuwa na tume huru ya uchaguzi, lakini kwa sasa siyo muda mwafaka kwa sababu wameshajiandaa kukabiliana na tume hiyo katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

"Tume huru ya uchaguzi tunaitaka wote kwa sababu ni ajenda kuu inayohusisha pia na mchakato wa katiba mpya, lakini kwa sasa kudai katiba mpya ni kujidanganya, muda umeenda na serikali haiwezi kuendesha mchakato huo wakati huohuo kujiandaa na uchaguzi," alidai. Katibu Mkuu wa Chama cha Wakulima (AAFP), Rashid Rai, alidai kitendo cha vyama vya upinzani kususia Bunge la Katiba kilihalalisha kuendelea kuwa na tume ya uchaguzi iliyopo sasa, hivyo vyama hivyo havipaswi kuilaumu serikali wakati wa lala salama.

Alidai ni wazi kuwa sababu za kudai tume huru ya uchaguzi ni baadhi ya wanasiasa kutaka madaraka na siyo kwa ajili ya kupata kiongozi bora wa kuongoza taifa.

Katibu wa Chama cha TLP, Richard Lyimo, alidai wanashangaa uamuzi wa Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, wa kuzuia mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 uliokuwa utolewe na Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kusaidia elimu nchini.

Lyimo alidai ni jambo la kusikitisha Zitto kushangilia serikali kukosa mkopo huo ambao ungesaidia wanafunzi wa familia zenye kipato duni kupata elimu na kwamba tafsiri yake anaunga mkono watoto hao kukosa elimu.

"Watanzania tunapaswa kuungana kulaani vitendo kama hivi vinavyofanywa na Zitto na Watanzania walioamua kuungana naye kumfuata huko kwa ajili ya kufurahia kukosa mkopo huo," alidai.

Katibu Mkuu wa Chama cha UDP, Saum Rashid, alidai kuruhusu watoto wa kike wanaopata ujauzito kuendelea na masomo ni kuhalalisha makosa yanayofanywa na vijana ya kukatisha ndoto za wanafunzi na kwamba kuna njia nyingi za kumaliza tatizo na siyo kuzuia mkopo.

Alisema Wizara ya Katiba na Sheria inapaswa kukazia adhabu ya sheria hiyo ili kumaliza tatizo hilo nchini badala ya Zitto kuzuia mkopo.

Hata hivyo, jana Zitto alinukuliwa na Nipashe akidai lengo lake siyo kuzuia mkopo huo bali kukomesha alichokiita ubaguzi dhidi ya wanafunzi wanaopata ujauzito shuleni.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiwa 'ameuchapa' usingizi katika eneo lake la biashara, Tandale, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania, Japan zaahidi kukuza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na Japan zimekubaliana kuendeleza uhusiano wa kidiplomasia na kushirikiana katika kuhakikisha maendeleo katika sekta za biashara, uwekezaji na viwanda baina ya nchi hizo mbili.

Akihutubia sherehe ya kumbukizi ya miaka 60 kuzaliwa Mfalme Naruhito wa Japan na Siku ya Taifa la Japan kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, Mkuu wa Itifaki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, alisema Tanzania na Japan zimekuwa na uhusiano mzuri wa kidiplomasia.

Alisema katika uhusiano huo, Japan imekuwa ikisaidia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile daraja la juu lililoko eneo la Tazara (Mfugale flyover) na mradi wa umeme wa Kinyerezi II.

"Kutokana na uhusiano mzuri baina ya Tanzania na Japan, serikali ya Japan imefadhili miradi mingine mbalimbali nchini ikiwamo ujenzi wa barabara ya Iringa - Dodoma, Dodoma - Babati, Tunduru - Namtumbo pamoja na upanuzi wa barabara ya Bagamoyo eneo la kuanzia Morocco hadi Mwenge," alisema.

Balozi Ibuge aliongeza kuwa mbali na ujenzi, pia Japan imefadhili miradi mbalimbali katika sekta muhimu nchini kama vile elimu, afya, maji na michezo.

"Serikali ya Japan imechangia sana suala la elimu. Watanzania wengi wamekuwa wakipata ufadhili wa kusomeshwa Japan mafunzo ya muda mrefu na yale ya muda mfupi na yamechangia kwa kiasi kikubwa ufanisi wa rasilimali watu," alisema.

Naye Balozi wa Japan nchini, Shinichi Goto, aliishukuru serikali ya Tanzania kwa umoja na mshikamano ambao imekuwa ikionyesha na kusema umekuwa chachu ya maendeleo kwa Tanzania na Japan.

"Urafiki wa kiuchumi kati ya Tanzania na Japan kwa sasa ni imara na ni matumaini yetu kuwa katika siku za usoni uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Japan utafikia hatua mpya ya ushirikiano," alisema.

# Serikali kutoa leseni bucha za nyamapori

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inaandaa kanuni kuruhusu matumizi ya nyama za wanyamapori na kutolewa kwa leseni ya kuanzishwa kwa bucha za nyama hizo, Bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, ambaye alisema mtalii anapoona na akatamani kula nyamapori itavutia zaidi.

"Je, serikali haioni umefika wakati iweke vigenge vya nyamachoma ndani ya hifadhi ili mtalii akiitamani nyama ile awe anaila?" Alihoji.

Pia alihoji kwa nini halmashauri au maeneo mengi yaliyozungukwa na hifadhi za taifa hazinufaiki na shughuli za utalii kwa kuwa hoteli zimejengwa ndani ya mbuga.

"Je, serikali haioni umefika wakati wa kuwekwa utaratibu wa hoteli zile ziijengwe nje ya hifadhi ili wananchi wanufaike na vitu mbalimbali kama kodi?" Alihoji

Akijibu swali hilo, Kanyasu alisema pia itaruhusiwa nyama hizo kutoka kwenye maeneo ya hifadhi za taifa na mapori ya akiba nchini ambapo wafanyabiashara watakwenda kuyachukua huko.

"Kanuni hizo pia zitaruhusu uwindaji wa ndani na kuruhusu kufunguliwa bucha ambazo zitakuwapo katka maeneo mbalimbali na kuzisajili. Hii itasaidia nyama hii ipatikane kwenye maeneo ya yote ya hifadhi na mapori ya akiba," alisema.

Alitolea mfano Hifadhi ya Taifa Serengeti nafasi ya kujenga hoteli imejaa na uzoefu unaonyesha kadiri hoteli zinavyojengwa ndivyo uharibifu wa mazingira unatokea na unaondoa uhalisia wa hifadhi.

"Kwa sasa tumekubaliana wawekezaji wapya tutawapeleka nje ya Hifadhi ya Serengeti na hifadhi nyingine zisizokuwa na nafasi ili kuvutia pia wananchi wanaozunguka maeneo hayo kuvutia biashara," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge Mlinga alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuongeza mapato ya utalii.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kanyasu alisema sekta ya utalii imeendelea kukua mwaka hadi mwaka.

"Idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,505,702 mwaka 2018. Katika kipindi cha mwaka 2018 pekee sekta hii imechangia katika uchumi wa nchi jumla ya Dola za Marekani bilioni 2.4 (sawa na Sh. trilioni 5.4)," alisema.

Alieleza kuwa sekta hiyo inachangia wastani wa asilimia 17 ya pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni.

"Aidha, inatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja milioni 1.6," alisema.

Kanyasu alisema mikakati inayotekelezwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini na mchango utokanao na sekta ni pamoja na kupanua wigo wa mazao ya utalii kijiografia kupitia Mradi wa REGROW.

Alieleza serikali inaendelea kufungua utalii katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kwa kuimarisha miundombinu ili kuboresha shughuli za utalii hususani katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Nyerere.



Wabeba mizigo wakihamisha saruji baada ya gari lililokuwa limebeba kupinduka katika eneo la Kibanda cha Mkaa Mbezi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ajiua gesti kisa msongo wa mawazo

INATOKA UK. 3

"Tulipofika tulivunja mlango na tulimkuta tayari amefariki dunia akiwa ametokwa na mapovu mdomoni," alisema.

Kamanda huyo alisema chanzo cha tukio hilo bado kinachunguzwa, lakini akadai kuna ushahidi kuwa alijiua kwa sumu ambayo haijafahamika kutokana na msongo wa mawazo kutokana na kufukuzwa kazi na mwajiri wake.

Alisema kuwa barua ya kufukuzwa kazi na mwajiri wake, ilitolewa Desemba 12, mwaka jana, akituhumiwa kuhusika na upotevu wa Sh. milioni 889 na kwamba mbali na kufukuzwa, pia mwajiri wake alimfungulia kesi mahakamani ambayo bado inaendelea. Malimi alisema mwaka jana baada ya Kachecheba kutuhumiwa kuhusika na upotevu wa fedha hizo, alifanya jaribio la kutoroka, lakini alikamatwa Bukoba na kurudishwa Ngara.

"Pia tulipofanya upekuzi katika chumba hicho tulikuta kifungashio ambacho ndani yake kilikuwa na dawa ambayo haijafahamika na chupa ya maji ya kampuni ya Bunena ambayo ndani yake haikuwa na maji na badala yake ilikuwa na kimiminika chenye rangi kama ya kijani na vitu vyeusi," alisema.

Mmiliki wa nyumba hiyo, Robert Katunzi, alisema alipewa taarifa na mfanyakazi wake kuwa mteja wao ambaye amekuwa pale kwa siku nne, hafungui mlango na hawana tena mawasiliano naye.

"Nilipopata taarifa hiyo nikamwambia wajaribu kumgongea tena asipofungua waende watoe taarifa polisi. Walifanya hivyo na polisi walipofika walivunja mlango ndipo ikabainika kuwa mtu huyo amejiua," alisema.

## JPM ahakikishiwa usalama wa Watanzania 400 corona China

INATOKA UK. 2

katika Jiji la Wuhan ambao wengi wao ni wanafunzi, hawajaambukizwa homa hiyo na jitihada za kuhakikisha wanakuwa salama zinafanyika.

Kwa upande wa Dk. Stergomena Tax, ilielezwa na Ikulu jana kuwa alikuja nchini kutoa taarifa ya utekelezaji wa masuala mbalimbali ya SADC ikiwamo uendelezaji wa viwanda na kanda huru ya biashara ambapo wamekubaliana kuendelea kuhamasisha nchi wanachama kuendeleza viwanda ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Alielezea baadhi ya maeneo yaliyopo katika mkakati wa kukuza uchumi wa SADC kuwa ni kuendeleza miundombinu hasa ya usafiri na nishati ambayo bado ni changamoto kwa nchi za SADC.

Aliipongeza Tanzania kwa hatua madhubuti zinazoendelea kuchukuliwa ikiwamo ujenzi wa barabara, reli na kuongeza uzalishaji wa umeme.

Kwa upande wake Balozi wa EU nchini, Manfred Fanti, alisema mazungumzo yake na Rais Magufuli yamekuwa na manufaa makubwa ambapo wamejadili maendeleo mazuri ya kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na EU, na kwamba katika siku za karibuni wamekamilisha mazungumzo yaliyoruhusu kuendelea kwa mpango wa EU kuchangia bajeti ya maendeleo ya Tanzania ambapo Sh. bilioni 132 zilizokuwa zimezuiwa, zimeruhusiwa na sasa wanaandaa mpango mwingine wa miaka saba utakaoanza mwaka huu.

Fanti alisema kwa jinsi anavyoyaona maendeleo ya Tanzania, ana matumaini makubwa kuwa EU itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na Tanzania ili kufanya vizuri zaidi.

Rais Magufuli alimshukuru Fanti kwa juhudi zake za kuimarisha uhusiano wa Tanzania na EU na akamhakikishia kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana na EU katika masuala mbalimbali yenye maslahi kwa pande zote mbili.

# Ujerumani yapiga jeki wanafunzi wenye ulemavu

**Na Sabato Kasika**

WANAFUNZI wenye ulemavu kutoka kata 10 za Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, wamepata msaada wa vifaa vya shule na vyakula, kutoka mradi wa BMZ wa nchini Ujerumani, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 16.

Kata zilizonufaika ni Bugwema, Bukima, Bukumi, Bwasi, Kiriba, Makojo, Murangi, Nyambono, Nyamrandirira na Suguti.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, Meneja wa Mradi wa BMZ, Niwaely Sandy, alisema vitu hivyo, ambavyo baadhi ya vifaa ni madaftari, mabegi na kalamu, vilitolewa hivi karibuni.

"Walemavu pia wamekabidhiwa vyakula kama mchele, mafuta ya kula na sukari, ambapo gharama ya vitu vyote vilivyotolewa na BMZ kwa kata hizo kumi inafikia Sh. milioni 16," alisema Sandy.

Meneja huyo alisema, Hospitali Teule ya Kanisa la Mennonite (KMT) la Shirati ni mdau wa mradi huo unaowezesha watu wenye ulemavu kutoka kata 10 za Musoma Vijijini na nyingine kumi za wilaya ya Rorya.

"BMZ ni neno la Kijerumani ambalo Kiingereza chake ni The Federal Ministry of Economic Cooperation and Development, kwa maana kwamba ni mradi wa serikali ya nchi hiyo," alisema Sandy.

Alisema, kwa kawaida shule zinapofunguliwa, mradi wa BMZ umekuwa ikitoa msaada huo kwa wanafunzi wenye ulemavu ili nao wapate elimu bila changamoto za ubaba wa vifaa vya shule.

"BMZ pia inahudumia na kutoa matibabu kwa watu wenye ulemavu kwenye wilaya mbili za Musoma na hasa kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini na Rorya, katika mkoani huu wa Mara," alisema.

# ATI yaleta maombi kuongeza uwekezaji nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA ilivyo kwa nchi nyingine za Afrika, Tanzania inawekeza katika uboreshaji wa miundombinu yake ili kukuza utalii na kuvutia wawekezaji.

Katika mazungumzo kati yake na serikali ya Tanzania, kampuni ya uwakala wa bima ya Afrika (the African Trade Insurance Agency - ATI) imetoa mapendekezo yatakayoisaidia nchi kuvutia wawekezaji.

Mapendekezo ya ATI pia yananuia kuisaidia nchi kupunguza gharama za kufadhili miradi ya baadaye kwa kati ya Dola za Marekani milioni 2 hadi Dola milioni 3 kwa mwaka kwa muda wa miaka kumi au zaidi.

Tanzania ni mwanachama mwanzilishi wa ATI. ATI ni taasisi ya kimataifa na ya kiafrika inayojishughulisha na kutoa dhamana za uwekezaji na mikopo ili kusaidia nchi wanachama kukuza viwango vya wawekezaji.

Katika mfumo unaopendekezwa ATI itatoa aina ya dhamana ya mikopo ijulikanayo kama 'credit wrap' kwa lengo la kusaidia nchi kupata unafuu wa riba inapopeleka maombiA ya mikopo katika soko la kimatAaifa.

Katika mfumo unaopendezwa (wa credit wrap), ATI imeshazisaidia nchi kadhaa za Afrika kupata mikopo kwa riba nafuu ambapo mwaka 2019, nchi za Benin na Côte d'Ivoire zilibahatika kupata mikopo inayofikia karibu Dola bilioni 1 (zaidi ya Sh. trilioni 2.3).

Mikopo hiyo itakuwa na riba za kiwango cha chini cha digiti moja (chini ya asilimia 10) na kulipwa kwa miaka zaidi ya 10 hadi 12.

Kwa muda mrefu, imekuwa ngumu sana kwa nchi za Afrika kupatiwa masharti nafuu kama haya ya mikopo.

Hii imetokana na ukweli kuwa ukanda wa Afrika huchukuliwa kuwa na hatari kubwa (high risk) ya mikopo kutokurudishwa kwa wakati na hivyo kwa muda mrefu ukanda huu umekuwa na upungufu wa bima ya mikopo.

"Lengo la ATI ni kuziba pengo hili la bima ya mikopo kwa kutoa dhamana zinazohitajika kwa nchi wanachama wake," alisema Tusekile Kibonde, Mkurugenzi wa kampuni ya wakala wa bima Tanzania (ATI) wakati wa mkutano na wadau wa maendeleo ya bima kubwa nchini uliofanyika Wizara ya Fedha na Mipango na kuratibiwa na ATI jijini Dodoma, jana.

Uwezo wa ATI kufanya kazi hiyo umepewa shime na uaminifu wake unaotokana na kupewa alama za juu za upimaji wa viwango vya uwekezaji uliofanywa na kampuni ya S&P and Moody's.

S&P and Moody's ni kampuni ya kimataifa ya utafiti na upimaji wa utoshelevu wa nchi au tasisisi katika kupata mikopo ya kimataifa.

Kwa miaka mitano iliyopita, ATI imeisaidia Tanzania katika maeneo kadhaa ya uwekezaji. Maeneo hayo ni katika mradi wa Sh. trilioni 2 wa ujenzi wa reli ya kisasa. ATI pia imesaidia katika maeneo mengine ya kuvutia uwekezaji katika sekta za fedha, nishati na miundombinu.

Ikiwa na uwekezaji wa Dola 447 milioni nchini, ATI inaamini kuwa ipo katika nafasi nzuri ya kuisaidia Tanzania kuongeza zaidi uwekezaji.

"Tukiwa benki inayoongoza kwa faida Tanzania, tupo pamoja na serikali kuchangia maendeleo endelevu kwa kubuni mifumo ya kisasa na kwa kushirikiana na wadau kama ATI ilikufikia malengo ya 2025 ya kiuchumi hususan kwenye miundombinu," alisema Mkuu wa Idara ya Huduma za Kifedha wa Benki ya NMB, Linda Teggisa.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa Benki ya CRDB, Prosper Nambaya, alisema ushirikiano kati ya benki yake na ATI umefanikisha ufadhali wa miradi mingi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu.



Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa Benki ya CRDB, Prosper Nambaya, akichangia mada wakati wa mkutano na wadau wa maendeleo ya bima kubwa nchini uliozishirikisha benki za ndani na kuratibiwa na Taasisi ya Africa Trade Insurance (ATI), jijini Dodoma juzi. Benki hiyo, imechangia maendeleo ya miradi mikubwa ya serikali ukiwamo mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge, uliopo Rufiji, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waelekezwa pa kupeleka migogoro ardhi

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

MSAJILI wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba nchini, Stela Tulo, amewataka wananchi kutumia vyombo vilivyo wekwa kwa mujibu wa sheria katika kutafuta haki kwenye migogoro ya ardhi.

Tulo alisema hayo katika maonyesho ya Wiki ya Sheria katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma. Alisema, kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi walio kwenye migogoro ya ardhi kwenda kwa viongozi kama wakuu wa mikoa, wilaya na viongozi wengine kutafuta haki kwenye migogoro ya ardhi, na kuacha vyombo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, jambo alilolieleza linachangia migogoro ya ardhi kutapata suluhu kwa wakati.

Kwa mujibu wa msajili huyo, vyombo vinavyohusika kisheria kutoa haki katika migogoro ya ardhi ni kuanzia ngazi ya Baraza la Ardhi la Kijiji, Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi na Mahakama ya Rufani. Alisema iwapo wananchi walio kwenye migogoro ya ardhi watafuata utaratibu wa kutumia vyombo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, wataweza kupata haki zao na wakati huo na kuepuka kupoteza muda mwingi wa kukata rufani kuhusiana na migogoro ya ardhi. Aidha, Tulo alitumia fursa ya maonyesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea kuwataka wananchi wa Jiji la Dodoma na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi kwenye maonyesho hayo ili kupata elimu kuhusiana na mabaraza ya ardhi, hivyo kujua taratibu za kutafuta wakati wa migogoro ya ardhi.

Naye Ofisa Ardhi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Arnold Mkude, alisema Ofisi ya Msajili wa Mabaraza ya Ardhi nchini inayatumia maonyesho ya Wiki ya Sheria kama njia ya kutoa elimu kwa wananchi wote wanaotembelea banda la ofisi hiyo ili kufahamu kazi na namna mabaraza ya ardhi yanavyofanya kazi.

## Ataka Tanzanite kuwa nyara taifa

MBUNGE wa Igunga (CCM), Dk. Dalali Kafumu, ameitaka serikali kutangaza madini ya Tanzanite kuwa ni nyara za Taifa itayovunwa na serikali pekee.

Akiuliza swali bungeni jana, Dk. Kafumu alisema madini ya Tanzanite yanapatikana nchini Tanzania pekee na juhudi za kufanya madini hayo kuchimbwa na Watanzania pekee kwa kanuni za madini za mwaka 2004 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 hazijaweza kuzaa matunda.

"Je, kwa nini Tanzania isiyatangaze madini ya Tanzanite kuwa ni nyara za Taifa itayovunwa na serikali pekee ili kuongeza manufaa ya kiuchumi kwa Taifa letu?" Alihoji.

Pia alihoji ni kwa nini serikali isiende kujifunza nchini Zimbabwe kuona jinsi ilivyofanikiwa kuyafanya madini ya almasi kuwa nyara ya serikali na hivyo kuleta manufaa makubwa sana kwa nchi hiyo.

Akijibu, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema ushauri wa kuyafanya madini ya Tanzanite kuwa nyara za Taifa na kwenda nchini Zimbabwe kujifunza utazingatiwa ili kuendelea kuboresha sekta ya madini kwa ujumla.

Alifafanua kuwa serikali inatambua upekee na umuhimu wa madini ya Tanzanite.

"Kwa muktadha huo, ilipelekea tarehe 20/9/2017 kuliamuru Jeshi la Wananchi Tanzania kujenga ukuta wenye urefu wa kilometa 24.5 kuzunguka eneo hilo ili kudhibiti utoroshwaji wa madini ili kupata manufaa stahiki ya kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla," alisema.

Alieleza kuwa eneo la Mirerani ambapo Tanzanite inapatikana lilitangazwa kuwa eneo lililodhibitiwa kwa tangazo la serikali namba 450 ya mwaka 2002.

"Lengo la hatua hiyo ni pamoja na kuthamini upekee na umuhimu wa madini hayo na kudhibiti upotevu wa mapato yanayotokana wa madini ya Tanzanite ili kuongeza manufaa kwa nchi," alisema.

Aidha, alisema madini ya Tanzanite yanachimbwa na Watanzania katika vitalu A, B, D na D-extension.

"Kitalu C kimekuwa kikichimbwa kwa ubia kati ya Shirika la Madini la Taifa (Stamico) na Kampuni ya kigeni ya TanzaniteOne Mining Limited (TML). Hata hivyo, Desemba 23, 2019 Stamico na TML waliachia leseni yao na sasa eneo limerudishwa kwenye usimamizi wa serikali," alisema.

Biteko alisema baada ya kuachiwa kwa eneo hilo, utaratibu maalum unaandaliwa wa namna bora ya kuligawa kwa kutoa leseni za uchimbaji wa kati kwa Watanzania wenye uwezo ili kuongeza mchango wa Watanzania katika uchumi wa madini.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Mbunge ahoji ugonjwa wa akili

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amesema asilimia moja ya Watanzania wana matatizo ya akili licha ya kwamba bado serikali haijafanya utafiti kujua takwimu halisi za tatizo hilo.

Dk. Ndugulile alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kemilembe Lwota. Katika swali lake, Mbunge huyo alisema utafiti wa nchi mbalimbali ikiwamo Marekani inaonyesha katika kila watu wanne, mmoja ana ugonjwa wa akili, Uingereza kwa kila watu watano mmoja ana tatizo la akili. "Mheshimiwa Spika nadhani hata wewe ni shahidi hata humu ndani wakati mwingine tunajiuliza tupo salama kiasi gani, nataka kufahamu serikali imefanya utafiti kujua ni watu wa ngapi wanakabiliwa na tatizo la akili Tanzania, na matokeo yakoje?" Alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri huyo alikiri kuwa matatizo ya afya ya akili yanazidi kuongezeka na kwamba Shirika la Afya Duniani (WHO) limeweka msukumo katika kuliangazia tatizo hilo. "Takriban asilimia moja ya jamii ya Watanzania tunaamini wana matatizo ya akili, inawezekana hata humu ndani tunachangia kwenye hiyo asilimia moja, tuna changamoto kama hizo," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali bado haijafanya utafiti wa kina kuangalia uzito wa jambo hilo ukoje na aina ya magonjwa ya akili yaliyopo nchini.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema ukatili dhidi ya wanawake na watoto bado unaendelea kwa kiwango kikubwa hapa nchini.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuwahudumia kwa unasihi na unasaha wahanga wa ukatili," alihoji. Akijibu swali hilo, Dk. Faustine alisema serikali inatambua uwepo wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini.

"Kwa kuliona hilo, serikali iliandaa mpango kazi wa kitaifa wa miaka mitano wa kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambao unatekelezwa kwa kipindi cha (2017/18 - 2021/22)," alisema. Alibainisha mpango mkakati huo unaainisha mikakati mbalimbali ya kupambana na kudhibiti ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. "Serikali imeanzisha vituo 11 vya mkono kwa mkono (One stop centres) kwenye mikoa ya Dare es Salaam, Pwani, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Arusha, na Simiyu kwa ajili ya kuwahudumia waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto," alisema.

Alieleza kuwa katika vituo hivyo, huduma za kipolisi, ushauri nasaha na huduma za afya zinatolewa kwenye kituo kimoja. "Lengo la serikali ni kuwa na kituo angalau kimoja kwa kila mkoa na hii inaenda pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu katika eneo la utoaji huduma husika," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na mwanafunzi, Elyn Michelle Mgunda, wakati wanafunzi wa darasa la nne wa shule ya Dar es Salaam Independent, walipotembelea Bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magunia 500,000 mkaa Dar kila siku

BUNGE limeelezwa kuwa mkaa unaoingia katika Jiji la Dar es Salaam kila siku ni wastani wa magunia 400,000 hadi 500,000 huku matumizi ya kuni na mkaa nchini ni zaidi ya asilimia 71.

Kufuatia hali hilo, serikali imeendelea na mikakati yake ya kuhakikisha gesi asilia inatumika majumbani ili kupunguza uharibifu wa mazingira ambapo watu 600 wameanza kutumia gesi hiyo.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Mollel.

Mbunge huyo alihoji jitihada za serikali katika kulinda misitu na mikakati ya haraka wa matumizi ya gesi ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Akijibu, Waziri Kalemani alisema wiki iliyopita ameunganisha gesi kwa wafanyakazi 110 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni mkakati mzuri wa kupunguza uharibifu huo.

"Awamu ya pili tunaenda kwa mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kuanza kusambaza mitungi iliyoshindiliwa gesi na kujenga mabomba kwenye mikoa hiyo kuanza kusambaza katika vijiji vyote ikiwa ni mkakati wa kupunguza uharibifu wa mazingira," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni kwa namna gani Wakala wa Misitu (TFS) inashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, husu san wilaya katika kusimamia misitu hapa nchini.

Akijibu, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constatine Kanyasu, alisema kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya Rasilimali za Misitu Tanzania ya mwaka 2015, Tanzania ina rasilimali za misitu zinazokadiriwa kufikia hekta milioni 48.1, ambapo asilimia 34.5 inasimamiwa na Serikali Kuu, asilimia 6.5 inasimamiwa na halmashauri.

"Pia asilimia 45.7 inasimamiwa na vijiji, asilimia 7.3 inasimamiwa na sekta binafsi, na asilimia 6 ya misitu iko katika ardhi huria. Kulingana na taratibu za serikali, misitu ya Tanzania inasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002," alisema.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, mamlaka za usimamizi wa misitu nchini zipo katika wizara mbili ambazo ni Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo imekasimu mamlaka hayo kwa TFS ambao una jukumu la kusimamia misitu ya hifadhi ya Serikali Kuu na misitu mingine yote ambayo haijahifadhiwa kisheria.

Kadhalika, alisema utafiti uliopo, misitu ya Tanzania inakabiliwa na matatizo makubwa mawili ambapo ni uharibifu mkubwa wa misitu unaofikia kiasi cha hekta 372,000 kwa mwaka na mahitaji ya mazao ya misitu kwa mwaka yanayozidi uwezo wa misitu kwa zaidi ya mita za ujazo milioni 19.5.

# Mvua yaua watatu na kuharibu miundombinu

**Na Allan Isack,** BABATI

MVUA zinazoendelea kunyesha mkoani Manyara, zimesababisha vifo vya watu watatu na kuharibu miundombinu ya barabara na makazi ya watu katika wilaya za Babati, Kiteto, Hanang' na Simanjiro.

Akitembelea maeneo yaliyoharibiwa na mvua hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema mvua imesababisha madhara makubwa kwa wananchi.

"Mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya mkoa huu imesababisha madhara ya kuharibu miundombinu ya barabara na kusomba makazi ya wananchi," alisema.

Mbunge wa Babati, Mjini Pauline Gekul, pia alitembelea maeneo hayo juzi na kuwataka wananchi kuwa makini kipindi hiki cha mvua kubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, aliwataka wakazi wa eneo hilo, kuchukua tahadhari wakati huu wa msimu wa mvua.

Katika Wilaya ya Hanan'g, daraja dogo kwenye barabara ya Katesh-Haydom limesombwa na maji.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Joseph Mkirikiti, alisema Wakala wa Barabara Vijijini (Tarura), umefika katika eneo hilo na umeanza utaratibu wa ukarabati wa daraja hilo.

Mkazi wa Kijiji cha Terrat wilayani Simanjiro, Elias Mollel, alisema makazi yake yamebomoka kutokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi.

"Mimi na familia yangu tunaishi kwa jirani, nyumba imebomoka baada ya mvua ya jana usiku," alisema.

Diwani wa Terrat, Jackson Ole Materi, alisema mvua hiyo, pia imekata mawasiliano kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwenye kata hiyo.

Materi alisema miongoni mwa waliopata adha kutokana na mvua hiyo, ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Terrat, walioshindwa kwenda nyumbani kwao kutokana



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (wa pili kulia), akizungumza na wananchi alipofanya ziara ya kutembelea kukagua vyanzo vya maji vilivyopo wilayani humo, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Bil. 5/- kujenga barabara Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha, imetia saini mikataba miwili yenye thamani ya Sh. bilioni 5.35 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 3.9.

Mikataba hiyo ilitiwa saini jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, Naibu Meya wa Jiji hilo, Paulo Matthysen, na Mkandarasi wa Kampuni ya China ya Sinohydro, atayejenga barabara hizo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia sasa.

Akizungumza baada ya kutia saini mikataba hiyo, ikishuhudiwa na aliyekuwa Mstahiki Meya wa Jiji hilo, Kalist Lazaro, Dk. Madeni alisema ujenzi wa miradi hiyo utakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Kisongo (Bypass), yenye urefu wa kilometa 1.7, itayojengwa kwa ajili ya kupisha upanuzi wa eneo la Uwanja wa Ndege Arusha.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 1.25, ambazo zimetolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ili kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Arusha.

Dk. Madeni alisema mradi mwingine ni wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 4.4, kutoka Murieti hadi Baypass.

Naibu Meya wa Jiji Arusha, Matthysen, alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 4.1, na ukikamilika, utaondoa tatizo la msongamano wa magari kwa wakazi wa eneo hilo.

Aliyekuwa Mstahiki Meya wa Jiji hilo, Lazaro ambaye ni mwasisi wa miradi hiyo, alisema amefurahi kuona miradi hiyo, ikijengwa kwa kuwa kabla ya kuondoka katika nafasi yake ya uongozi, alishiriki katika upembuzi yakinifu, hivyo anajisikia faraja kuona miradi hiyo ikijengwa kwa kasi kubwa.

"Nashukuru kwa heshima niliyopewa na uongozi wa jiji kuona miradi niliyoshiriki kuiasisi ikianza kujengwa kwa kasi chini ya usimamizi wa Jiji la Arusha," alisifu.

Mkandarasi wa Mradi wa Barabara hizo kutoka Snohydro, Lang Shang, alisema kampuni hiyo inatarajia kukamilisha mradi huo kwa wakati lakini kwa kipindi hiki wanakwamishwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Meneja wa Uwanja wa Ndege Arusha, Elipid Tesha, alisema Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetoa eneo la uwanja wa ndege ili kujengwa barabara ya mchepuko ya Kisongo yenye urefu wa kilometa 1.7.

Alisema upanuzi wa uwanja huo utaruhusu ndege kubwa kutua na kuruka katika uwanja huo, zikiwamo za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

## CCM yaridhishwa utekelezaji Ilani

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Arumeru ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Arusha.

Wajumbe hao walifanya ziara katika miradi ya maendeleo ya Tarafa ya Moshono, ikiwa ni sehemu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

Wajumbe hao wamesema wameridhishwa na ubora wa ujenzi wa miradi waliyoikagua, wakiipongeza serikali kwa utendaji wake.

Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Arumeru, Simon Ole Saning'o, alisema wameona mapinduzi makubwa ya kimaendeleo, yaliyofanywa na serikali kwa wananchi kwa kipindi cha miaka minne chini ya Rais John Magufuli.

Saning'o alisema serikali imetekeleza Ilani ya CCM kwa zaidi ya asilimia 90, kwa kujenga miradi mikubwa katika sekta za elimu, afya, maji, umeme na miundombinu ya barabara.

"Rais Magufuli alipoingia madarakani, alikabidhiwa Ilani ya CCM, iliyojikita kwenye kuendeleza sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara, umeme na kilimo.

"Kwa kipindi kifupi cha miaka minne, serikali imefanya mapinduzi makubwa katika utekelezaji wa Ilani tofauti na vipindi vilivyopita," alisifu.

Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na wa ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Sokoni II, uliogharimu Sh. milioni 190 kwa ufadhili wa Ubalozi wa Japan nchini.

Mradi mwingine uliotembelewa ni ujenzi wa maktaba na ukarabati wa bwalo la chakula katika sekondari ya Mlangarini uliogharimu Sh. milioni 140, ujenzi wa darasa moja katika Shule ya Sekondari Olokii kwa nguvu za wananchi na ujenzi wa Kituo cha Afya Nduruma Sh. milioni 500.



# TRA yatakiwa kuimarisha ushirikiano

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imeiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani humo kuongeza ushirikiano na taasisi nyingine za serikali pamoja na vyombo vingine ili kupiga vita ukwepaji wa ulipaji wa kodi.

Aidha, uongozi wa mkoa huo umeagiza TRA kuweka mfumo mzuri wa udhibiti wa wakwepa kodi huku ukisisitiza wakwepakodi wachukuliwe hatua za kisheria.

Mkuu wa Mkao wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema hayo jana wakati akizungumza namna ambavyo serikali itashirikiana na mamlaka husika kuhakikisha kila anayestahili kulipa kodi anafanya hivyo.

Alisema vitendo vya ukwepaji kodi vinachangia kukwamisha malengo na mipango ya maendeleo ya serikali hivyo vinapaswa kudhibitiwa.

"Imarisheni ukaguzi wa kumbukumbu za walipa kodi ili kutambua kodi iliyo kwepwa hakikisheni pia mnakusanya malimbikizo yote ya kodi ambayo hayajakusanywa ili kila mmoja atambue umuhimu wa kulipa kodi ni muhimu mfumo wa kodi ufahamike kwa wananchi wote," alisema.

"Maofisa wa TRA nawakumbusha hakikisheni mnachunguza na kuwatambua wafanayabiashara ambao hawalipi kodi na kuwaongeza kwenye wigo la walipa kodi," alisema.

Aidha, aliwataka kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuwakadirio yaliyo sahihi na kuepuka lugha chafu na kutomwelewesha mteja mara anapofika katika ofisi zao.

Kaimu Meneja wa TRA mkoani Kilimanjaro, Rashid Herith, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika ukusanyaji wa kodi ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kutokulipa kodi kama inavyostahili jambo ambalo linaikosesha serikali mapato.

"Baadhi ya wafanyabiashara hawatoi risiti za mauzo na wengi hawalipi kodi kama inavyowapasa na hivyo kuikosesha serikali mapato yake hivyo natoa rai kwa wananchi kudai risiti pale wanaponunua bidhaa," alisema.

Aidha, alisema wamejiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwamo kupambana na biashara haramu za magendo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusiana na sheria za kodi hususani zile za msingi.

"Tutaongeza juhudi ya kufuatilia na kukusanya malimbikizo ya kodi, kutoa elimu ya kodi kwa wadau wetu, kupanua wigo wa kodi kwa kutembea mtaa hadi mtaa na pia tutaimarisha ukaguzi wa kumbukumbu za walipakodi mara kwa mara," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) mkoani humo, Hillary Lyatuu, alisema ikiwa mazingira ya mlipa kodi yataboresha ikiwa ni pamoja na kutoa elimu lugha nzuri kwa wafanyabiashara mapato yatapatikana.

"Hali ya kuimarisha mazingira ya uanzishwaji wa biashara inaendelea kuwa nzuri ingawaje baadhi ya wafanyabiashara wamehamishia baishara zao sehemu nyingine nchi nyingine na wengine kufungwa kabisa jambo hili lifanyiwe kazi kutafuta ufumbuzi," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mngwira, akijaza mafuta bodaboda kuashiria uzinduzi wa kituo kipya cha mafuta na huduma cha Total Kilimanjaro, katika kijiji cha Samanga, kilichopo Marangu mkoani Kilimanjaro ambacho kinamilikiwa na mfanyabiashara mzawa kwa asilimia 100, ila kimejengwa kwa ushirikiano na kampuni ya mafuta ya Total Tanzania katika utaratibu unaitwa DODO. Nyuma yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Jean Franchois Schoepp, na Meneja wa Mtandao wa vituo vya mafuta vya Total, Marriame Sow na mke wa mmiliki wa kituo hicho, Eliawony Towo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanyama waharibifu wavitesa vijiji

**Na Mary Mosha,** SIHA

WANANCHI wa vijiji vitano wilayani Siha, vilivyopo Msitu wa Nusu Maili, wameeleza jinsi wanyama kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa) wanavyowaumiza kwa kuharibu na kula mazao yao kiasi cha kusababisha njaa.

Vijiji hivyo ni Ngarony, Sherehe, Mowo Jamu, Messe na Samaki Maziwa. Wakizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Ngarony, Benson Kileo, kwa niaba ya wenzake, alisema wanyama hao wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa katika mashamba hali ambayo inaweza kusababisha wakazi hao kukumbana na baa la njaa.

Aliwataja wanyama wasumbufu ni kama tembo, nyati, nguruwe pori, nyani pamoja na tumbiri, wamekuwa wakishuka mara kwa mara na kutafuna mazao yao yaliyopo mashambani hasa katika kipindi cha Machi hadi Mei kila mwaka.

Harison Marisha, mkazi wa Samaki Maziwa, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, serikali iangalie uwezekano wa kuwadhibiti wanyama hao pamoja na kuwapa wananchi mbegu za mazao wengine ambayo hayatashambuliwa na wanyama pori ikiwa kutakuwa na uwezekano huo.

Mhifadhi Msaidizi wa Kinapa, Charles Ngenda, alisema wanyama wanaingia kwenye mashamba ya wananchi kutokana na hali ya hewa nzuri na mazingira yaliyotulivu yaliyotokana na utunzaji wa mazingira.

Alisema, hali hiyo inawafanya wanyama hao kujongea katika mashamba ya wananchi na kuleta uharibifu mkubwa unaoweza kuwasababishia madhara, lakini mara wanapowaona wanyama hao watoe taarifa hiyo na maofisa wa husika watafika eneo husika na kuwafukuza wanyama hao ili kuepuka madhara hayo.

"Ni kweli wanyama hufuata mazingira yaliyo tulivu, lakini tumechukuwa kama changamoto na tutaifanyia kazi ili kutatua kero za wananchi hao," alisema Ngenda.

Mkuu wa Wilaya Siha, Onesmo Buswelu, aliwataka wananchi hao kuwa wavumilivu wakati serikali ikishirikiana na hifadhi kuhakikisha wanatatua changamoto hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, aliitaka Kinapa kupitia ujirani mwema kukaa na vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro na kuangalia namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi hao.

## Fursa mpya ya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mafuta ya Total ya Tanzania imezindua kituo kipya cha mafuta na huduma cha mkoani Kilimanjaro, eneo la Marangu ambacho kitauza mafuta, vilainishi na kutoa huduma ikiwamo kufanya huduma za magari.

Uzinduzi wa kituo hicho jana ni katika utekelezaji wa mpango wa biashara wa kampuni ya mafuta ya kampuni hiyo kupanua wigo wa biashara yake nchini katika kusambaza huduma nchi nzima.

Kituo cha Total Marangu, ni moja ya vituo vipya vya Total vinavyoendeshwa kwa ubia kati ya kampuni na mfanyabiashara mzawa (DODO), ambapo kituo hiki ni cha kwanza cha mfumo huu katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Alizungumza wakati wa uzinduzi wa kituo hiko, Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Jean Franchois Schoepp, alisema: "Total tumedhamiria kuwafikia Watanzania wengi zaidi kwa kuwapatia na fursa ya kupata huduma bora kutoka katika vituo vyetu vyenye mafuta bora ya Total Excellium na bidhaa zenye ubora.

Tunawaalika wafanyabiashara ambao wanamiliki vituo vya mafuta na wapo tayari kushirikiana nasi kuchangamkia fursa hii kupitia mpango wetu wa DODO. Tunajua mkoa wa Kilimanjaro ni mkubwa na una maeneo mengi muhimu ambayo Total hatujayafikia kama Rombo, Machame na Holili, hivyo ni matarajio yangu kuwa wafanyabiashara zaidi wa Tanzania watachangamkia fursa hii nzuri."

Tumefurahi sana na tunampongeza mmiliki wa kituo hiki, Eliawony Towo kwa ushirikiano nasi... tunatoa wito kwa wafanyabiashara wengine, kujitokeza ili kuwapa fursa zaidi Watanzania kufaidika na bidhaa," alisema Schoepp.

Alisema wanapopata wawekezaji wenye kutoa fursa kwa wafanyabiashara wazawa ya kushirikiana nao katika kuleta maendeleo.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 6, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



## Dawa mpya kukabili 'aleji' ya karanga

Ukurasa 14



SIKU MAALUM YA KWANZA

## Taasisi Ifakara yazindua rasmi kwenye hali mbaya Bagamoyo

Ukurasa 16



SIKU YA SARATANI

## Bosi Ocean Road aorodhesha aina 10 vinara kuitesa nchi

Ukurasa 20




Kaimu Mganga Mkuu wa Mwananyamala, Dk. Mussa Wambura, akizungumza na waandishi wa habari.

# HOSPITALI MWANANYAMALA IMEZALIWA UPYA KIUTENDAJI

Ukurasa 14



Karanga zilizokaagwa. **PICHA: MAKTABA.**

# Dawa mpya kukabili 'aleji' ya karanga

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE imegunduliwa dawa mpya aina yake kukabili mzio au 'aleji' ya matumizi ya karanga katika mlo, mahsusi kwa watoto.

Dawa hiyo iliyoko katika mfumo wa poda, ambayo baada ya kufanyika utafiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Chakula na Dawa ya Marekani, imeidhinisha kuanza kutumika rasmi kwa walengwa watoto wenye umri kuanzia miaka mine hadi vijana wa miaka minne na 17

Hata hivyo, katika matumizi hayo kuna angalizo linalotolewa, kuna uhitaji wagonjwa wenye tatizo la mzio wa karanga, kuendelea kuwa makini na ikiwezekana, kuwa mbali na matumi yake.

Nchini Marekani, hadi sasa kuna kundi kubwa la watu wenye matatizo hayo na wagunduzi wa dawa, wanasema hawajafikia hatua kujiamini wamelimaliza tatizo.

Mwaka jana, watafiti wanazuoni wa Chuo Kikuu cha King, kilichoko London, Uingereza walisema tiba ya mzuio huo,inaendana masharti ya ama kutumia kiasi kidogo au kuachana nayo kabisa.

Katika jamii nyingi, ikiwamo ya Kiafrika hasa katika maeneo yanakozalishwa karanga hutumika kwa namna nyingi, kama kutafuna mbichi na za kukaanga, za kusagwa na mafuta yake yanatumika kwa mapishi.

AFYA

# HOSPITALI MWANANYAMALA IMEZALIWA UPYA KIUTENDAJI

- Kondo uzazi inakuwa chanzo gesi
- Wizi watoto umejipiga marufuku
- Tiba kwa watumia 'unga' 1200

**Na Mary Geofrey**

KUNA miaka ya nyuma Hospitali ya Rufani Mwanayamala, mkoani Dar es Salaam, haikuwa na taarifa ya kupendeza kutoka na huduma, hata mengine ya kimazingira.

Itakumbukwa, kuna wakati hata Rais wa awamu iliyopita, Jakaya Kikwete, alihoji kwa uchungu kinachojiri hopitalini Mwananyamala, kubeba picha mbaya isiyobadilika,

Kwa ujumla, matukio yaliyokuwa yanatendeka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dar es Salaam ya Mwananyamala, yalitosha kuwa tishio kwa wajawazito na wazazi waliokuwa wakifika kupata huduma.

Kila kona ya Manispaa ya Kinondoni, Ubungo na eneo jirani zilizagaa habari kuwa 'hospitali hiyo inaiba watoto wachanga.'

Ukiacha habari za wizi wa watoto, wajawazito nao walilazimika kubeba ndoo za maji ya moto pindi wanapoenda kujifungua kwa ajili ya kuwakanda.

Ndoo iliyotumika kupelekea maji, wakati mwingine ilitumika kubeba kondo la nyuma la uzazi, kwenda kuteketezwa nyumbani.

Haya ni mambo makubwa ambayo yaliumiza vichwa vya viongozi wa serikali na watendaji wa hospitali hiyo kabla ya kuitwa Mwananyamala ya sasa, inayochukua sura mpya.

**UKWELI UKOJE?**

Mwandishi wa Nipashe kwa hatua amefuatilia sababu za changamoto hizo na kilichofanyika hadi kuwapo simulizi ya Mwananyamala mpya iliyoboreshwa.

Hatua tatu baada ya kuingia geti la Mwanyamala unakutana na askari wa Suma JKT wanaokupokea kwa kusimamisha chombo cha usafiri na kuanza kuhoji maswali yenye kumpa taarifa za kutosha ulikotoka, unakoenda na shida yako, kabla hawajalikagua gari kwa ufasaha.

Ni ukaguzi wa mwendesha gari na mtembea kwa mguu naye ana yake.

Kwa wote, majibu ya kutosheleza ndio yanayohusu ama ugeuze kurudi ulikotoka au upewe maelekezo wapi pa kuelekea, mara baada ya ukaguzi huo.

Tulielekezwa jengo la utawala ambako tulikutana na wenyeji wetu waliokuwa wakitusubiri, huku hewa safi ikiendelea kupuliza eneo hilo.



Kaimu Mganga Mkuu wa Mwananyamala, Dk. Mussa Wambura, akizungumza na waandishi wa habari.

> **"Kati ya changamoto zilizokuwa zinatusumbua hospitali ya Mwananyamala, ni hii tuliigeuza kuwa fursa kwetu na leo tunaona mafanikio makubwa tuliyo nayo," anasimulia Dk. Wambura.**

Ni tofauti iliyoanza kujionyesha kimazingira ya hewa safi, iliyozimngira.Ni tofauti sana na miaka ya nyuma, mazingira yalikuwa kinyume.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mwananyamala, Dk. Mussa Wambura, baada ya kuwapokea, anawaingiza wanahabari katika ukumbi mpya wa mikutano ya watumishi hospitalini.

Sylvester Omary, ni Ofisa Habari wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), aliyekuwa kiongozi wa msafara siku hiyo, kwa niaba ya Ofisa Habari Mwandamizi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura.

Anatumia fursa hiyo kutambulisha ujio wa maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na timu ya wanahabari waliofika hapo, kuangazia mafanikio ya sekta ya afya katika taasisi zake katika kipindi cha miaka minne serikalini.

Kaimu Mganga Mkuu, Dk. Wambura, akiwa Mkurugenzi Huduma za Matibabu wa Mwananyamala, Dk. Isdory Kiwale wanaanza kuelezea hospitali hiyo ilikotoka, ilipo na inakoelekea.

**KONDO LA GESI**

Dk.Wambura anasema, Mwananyamala inatoa huduma kwa wanawake 40 hadi 60 wanaojifungua kwa siku sawa na jumla ya 900 hadi 1,200 kwa mwezi, idadi inayoongezeka kulingana na msimu.

Anasema kutokana na idadi hiyo, kubwa inaendana na makondo ya nyuma ya uzazi yanayozalishwa kwa siku, hali iliyowafanya kutumia mtambo kuteketeza kwa moto.

Dk. Wambura anasema:"Wakati mwingine mtambo ulizidiwa au kuharibika, tulilazimika kuwapa wazazi wakateketeze nyumbani ili kuepuka changamoto ya uchafu wa mazingira ikiwamo harufu kali."

"Kati ya changamoto zilizokuwa zinatusumbua hospitali ya Mwananyamala, ni hii tuliigeuza kuwa fursa kwetu na leo tunaona mafanikio makubwa tuliyo nayo," anasimulia Dk. Wambura.

Anasema jambo la kwanza walibuni namna bora ya kuteketeza kondo hilo, ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuigeuza fursa ya kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa Dk. Wambura, walifanikiwa kufunga mtambo wa kisasa wa kutumia kondo hilo kuzalisha gesi kwa ajili ya kuchemshia maji ya wazazi wanaojifungua katika hospitali hiyo.

Dk. Wambura anasema, huduma hiyo ilianza mwaka 2018 baada ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), iliponunua na kufunga mashine isiyopatikana katika hospitali yoyote nchini, zaidi ya Mwananyamala.

Anasema, kutokana na kuwapo huduma hiyo, kumemaliza changamoto ya wanawake kubebeshwa ndoo za maji ya moto kutoka nyumbani na kondo walilokuwa wakifungashiwa kurudi nayo nyumbani kuyatupa.

"Mwananyamala tuliamua kutumia changamoto zilizokuwa hospitalini hapa kama fursa, baada ya wizara kutuletea kifaa hiki muhimu.

"Tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kumaliza changamoto waliyokuwa wakipata ndugu wa wanawake waliojifungua ya kuja na ndoo za maji ya moto ya

**Inaendelea Uk. 15**

AFYA

Inatoka Uk. 14

# HOSPITALI MWANANYAMALA IMEZALIWA UPYA KIUTENDAJI

kuwakanda na wakati wa kuondoka tuliwabebesha kondo wakayateketeze nyumbani," anasema Dk.Wambura.

**MKURUGENZI TIBA**

Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu, Dk. Kiwale, anasema mashine hiyo ina ujazo wa gesi 308, inayoweza kutumika kupika na kuwasha taa za hospitali.

Anasema kiasi cha gesi inayotumika kuchemsha maji ni ndogo kulinganisha na uzalishaji, hivyo wana mpango wa kuitumia kwa ajili ya taa za wodi ya wanawake na kupikia katika jiko la hospitali hiyo.

"Kutokana na kuwa gesi inayozalishwa ni nyingi na kama tulivyoeleza kwa siku wanawake 40 hadi 60 anajifungua, ina maana tunazalisha gesi ya kutosha na hatuwezi tukaiuza nje ya hapa," anasema Dk. Kiwale.

Kwa siku za baadaye tunatarajia kuitumia kwa ajili ya taa za wodi za wanawake na kwenye kantini ya hospitali," anaendelea

**UIBAJI WATOTO**

Kaimu Mganga Mkuu wa Mwananyamala, Dk. Wambura, anasema changamoto nyingine kubwa iliyowatesa, ni wizi wa watoto ambayo anajigamba sasa wameimaliza na imetimu miaka minne na sasa hakuna mtoto anayeibiwa.

Anasema, upoteaji watoto wachanga katika hospitali hiyo iliwaumiza vichwa sana, hivyo walibuni mbinu za kukabiliana nayo, ikiwamo kuwaondoa wafanyakazi wote wa mochuari walioonekana kuwa chanzo cha tatizo hilo na kubadili askari wote.

"Tulibaini walikuwa wakipotea, kwa sababu kulikuwa na watumishi wasiokuwa waadilifu walioshirikiana na wahalifu," anasema Dk. Wambura na kufafanua, walichukua hatua ya kuondoa walinzi wote waliokuwa wakilinda eneo lote la hospitali na sasa linalindwa na askari wa Suma JKT.

Anasema, pia walifunga mlango wa nyuma wa hospitali hiyo ambao awali ulitumiwa, hivyo watu wasiyo waadilifu waliutumia kufanya uhalifu na badala yake sasa unatumika kutolea na kuingiza maiti peke yake.

"Wahalifu na watumishi wasiyo waadilifu walitumia kufanya uhalifu huo kwa sababu haiwezekani kabisa, mtoto anapotea wodini wakati mzazi akiwa chini ya uangalizi wa madaktari na manesi.

Kwa sasa hivi, uhalifu umemalizika kabisa kwa sababu hamna namna unaweza kupita geti kubwa na mtoto au kitu chochote bila kubainika," anasema Dk.Wambura.

Dk. Kiwale, anatoa ufafanuzi kuwa baadhi ya watumishi waliobainika kuhusika na uhalifu huo, walichukuliwa hatua za kinidhani, hali iliyosaidia kumaliza changamoto iliyokuwapo.



Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu wa Hospitali ya Mwananyamala, Dk. Isdory Kiwale, akionyesha mashine inayotumika kuzalisha gesi kwa kutumia kondo la nyuma la uzazi. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY**

> **"Wahalifu na watumishi wasiyo waadilifu walitumia kufanya uhalifu huo kwa sababu haiwezekani kabisa, mtoto anapotea wodini wakati mzazi akiwa chini ya uangalizi wa madaktari na manesi.**

Anataja lingine, ni kwamba wameimarisha ukaguzi katika mlango mkuu wa kuingia na kutokea na eneo lote la hospitali, kuweka mbali uwekezeno au kuwapo uhalifu.

Mkurugenzi huyo wa huduma, anasema pia wanapokea ripoti ya hospitali kila siku asubuhi, zinazosaidia kufahamu hali ya usalama na kiwango cha tija ya huduma zinazotolewa kila siku hospitalini.

**UZALISHA MIFUKO**

Dk. Kiwale anasema hospitali hiyo hivi sasa ina mtambo wa kuchakata chupa na mifuko ya plastiki, kutengeneza mifuko ya kuhifadhi taka za hospitali.

Anafafanua kuwa, ni huduma inayosaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuzalisha mifuko hiyo ya kuhifadhia taka za hospitali, hata kuifanya ipunguze gharama zisizo za lazima kwa uendeshaji wake.

Mkurugenzi huyo anasema, mifuko yote inayotumika kuhifadhi taka hospitalini, wanalishwa wenyewe na imefikia hatua inasaidia uwezekano wa kutumiwa na hospitali nyingine.

**DAWA ZA KULEVYA**

Dk. Wambura anaeleza katika huduma za kuwasaidia waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya, akisema wana kituo kinachohudumia na sasa imeimarika na idadi ya vijana wanaofika kupata huduma, imeongezeka kutoka 12,000 hadi 19,000.

Anasema kutokana na vijana kuacha kutumia dawa za kulevya na kutumia mbadala dawa za methadone, idadi ya wahalifu imepungua kwa mujibu wa takwimu zilizofanywa na hospitali hiyo.

Dk. Wambura anasema, idadi ya majeruhi mbalimbali wa kuchomana visu na vitu vyenye nchi kali, imepungua kwa sababu waliokuwa wanafanya uhalifu huo wengi ni watumiaji wa dawa.

Anaeleza kuwa huduma za matibabu katika hospitali hiyo zimeimarika kutokana na kuwa na madaktari bingwa wa kutosha 24 wanaotoa huduma kwa saa 24, pia idadi ya wagonjwa wanaotibu imeongezeka kutoka 1,400 hadi 2,500 kwa sasa.




Jengo jipya la upasuaji kwa wajawazito katika Hospitali ya Rufani Mwananyamala. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

SIKU MAALUM YA KWANZA

# Taasisi Ifakara yazindua rasmi kwenye hali mbaya Bagamoyo

- Matende, trakoma, usubi, kichocho balaa
- Kotonawa uso tatizo...minyoo tumbo 28.5%
- Hakuna aliye salama; wakazi walia pia 'UTI'



Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo, Kasilida Mgeni, akizungumza katika uzinduzi wa Siku ya Kitaifa ya Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele, Alhamisi iliyopita.

**Na Beatrice Philemon**

KATIKA jamii kuna magonjwa yasiyopewa kipaumbele. Hapo kuna maradhi kama minyoo ya tumbo, kichocho na ngiri maji. Serikali imeamua 'kuivalia buti.'

Hivi sasa, Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), imeamua kuipigia kambi wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani kutoa elimu kwa jamii kuhusu maradhi hayo, hatua inayoendana na kuwashauri wananchi kumeza dawa kwa ajili ya kinga na tiba.

Ni kwamba imebaini hali ya kuwepo imani potofu, bado wananchi hawataki kumeza dawa, kwa dai kwamba 'dawa hizo zinamaliza nguvu za kiume' na dai hilo linashusha imani na misimamo shuleni, wazazi wakiwakataza watoto wao kwamba zinawadhuru

Akizungumza na Nipashe katika uzinduzi wa tarehe maalum ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele duniani, ambayo ni Januari 30 ya kila mwaka, katika Shule ya Msingi Nia Njema, mtafiti, Dk. Michael Mihayo, anawataka wananchi wabadilike kuhusu ugonjwa huo na yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.

**"Wananchi wajitokeze kumeza dawa hizi na tunaomba wazazi wasiwazuie watoto kunywa dawa za minyoo na kichocho, kwa sababu dawa hizi ni salama hazina madhara yoyote kwa afya zao, zimethibitishwa na wizara ya afya na Shirika la Afya Duniani (WHO)," anasema.**

Dk. Mihayo anataja maradhi mengine katika orodha hiyo iliyokosa kipaumbele, ni pamoja na: Matende, trakoma, usubi, kichocho, minyoo ya tumbo na kichaa cha mbwa.

"Tuache imani potofu," anatamka Dk. Mihayo na kuiasa jamii ya Bagamoyo: "Mkipata magonjwa kama haya, mhudhurie kwenye vituo vya afya vinavyotoa dawa hizo, pia mshiriki kunywa dawa hizo."

Anasema, Taaasisi ya Afya Ifakara inafanya kazi hiyo kwa niaba ya serikali, ikiwamo katika shule za msingi na maeneo ya mijumuiko. Anawakumbusha wananchi kwamba wako hatarini kuambukizwa maradhi hayo, ambayo yameshawafikia watu takriban milioni tano.

"Wananchi wajitokeze kumeza dawa hizi na tunaomba wazazi wasiwazuie watoto kunywa dawa za minyoo na kichocho, kwa sababu dawa hizi ni salama hazina madhara yoyote kwa afya zao, zimethibitishwa na wizara ya afya na Shirika la Afya Duniani (WHO)," anasema.

Anasema shughuli hiyo imetengewa siku ya Januari 30 kila mwaka, ikiwa ni kumbukumbu ya Azimio muhimu la 2012 London, nchini Uingereza kwa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.

Dk. Mihayo anasema, ilisaidia kuwaunganisha washirika kutoka sekta tofauti katika nchi na jamii za magonjwa haya kushinikiza uwekezaji mkubwa na kuchukua hatua.

**KULIVYO BAGAMOYO**

Anasema, wilayani Bagamoyo ugonjwa wa minyoo ya tumbo na kichocho unaongoza kwa kuathiri watoto wa shule za msingi na walio na chini ya miaka mitano.

Dk. Mihayo anaainisha takwimu kwamba, minyoo ya tumbo inaongoza kwa asilimia 28.5 ya watoto wote, kichocho asilimia 0.2 na ngirimaji inaongoza kwa asilimia 0.2, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti uliyofanyika mwaka 2015 katika vijiji vya Kiwangwa, Msata, Mkange na Magomeni, wilayani Bagamoyo.

Kutokana na tatizo hilo, anasema kati ya mwezi ujao na Mei, Taasisi ya Afya Ifakara inatarajia kutoa dawa za minyoo ya tumbo na kichocho, ikirejea rai kwa wazazi wasiwazuie watoto kunywa dawa hizi, kwani ndio chanzo cha changamoto kwa utekelezaji operesheni hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mihayo, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele duniani, yamepewa siku maalum kila mwaka itakayosaidia wadau wa afya duniani, ikiwamo Tanzania, kuwa na namna ya kuhamasisha hatua za tahadhari, hasa katika nchi na jamii zilizoathiriwa zaidi na magonjwa hayo.

Pia, inaelezwa kuwapo siku maalum kutasaidia kuwaleta pamoja wadau wakiwamo viongozi, asasi za kiraia, wataalam wa afya duniani na watunga sera wakiunganishwa kutokomeza magonjwa hayo.



Kikundi cha ngoma kutoka Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (Tasuba), wakitumbuiza katika uzinduzi wa Siku ya Kitaifa ya Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

"Mwaka huu wa 2020 utakuwa ni mwaka wa uamuzi wa magonjwa hayo na mwanzoni wa mwaka huu 2020, Shirika la Afya Duniani(WHO), linatarajiwa kuzindua malengo mapya ambayo yataonyesha jinsi ya kupambana na magonjwa haya," anasema.

Dk. Mihayo anainisha kwamba, katika wananchi wote nchini wanaokadiriwa kuwapo wastani wa milion 53, wapo hatarini kuambukizwa maradhi hayo yasiyopewa kipaumbele na katika kundi hilo, milioni tano wameshathirika kwa mojawapoo ya maradhi hayo.

Mbali na hilo, magonjwa hayo yamekuwa na madhara makubwa katika Jamii yetu.

**KATIBU TAWALA**

Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo, Kasilida Mgeni, aliwataka wananchi waliokusanyika Alhamisi iliyopita

kwa ajili ya uzinduzi huo, ambao ni mara ya kwanza duniani, waathirika zaidi ni jamii masikini, huku madhara yenyewe yakikua taratibu.

Hadi sasa, taarifa za WHO zinakadiria watu bilioni moja duniani kote wameshaathirika na wengine bilioni mbili wako hatarini kuambukizwa, hali inayomfanya kila mtu kuwa na wajibu wa kujikinga nayo

"Njia za kujikinga na magonjwa haya, ni kutumia dawa za kutibu na kudhibiti magonjwa hayo, ambayo hutolewa kila mwaka na serikali na kuzingatia usafi wa uso kwa kunawa angalau mara mbili kwa siku na usafi wa mwili kwa ujumla," anasisitiza.

Kasilda anataja lingine, ni matumizi sahihi ya choo na usafi wa mazingira kwa kujiepusha na kuoga, kuogelea na kutembea bila ya viatu kwenye maji yasiyo safi au yaliyotuama kama vile kwenye mabwawa na mifereji.

Anataja eneo lingine ni kujikinga na kuumwa na nzi, mbu, wadudu wasambazao magonjwa haya na kutibiwa haraka mara baada ya kuona dalili au kugundulika na ugonjwa

"Pia tukumbuke kuwa ni wajibu wetu mkubwa kuwapeleka watu wote wenye dalili za magonjwa hayo katika vituo vya huduma, ili wafanyiwe uchunguzi na kupewa matibabu kabla hawajapata madhara makubwa, ambayo yatawafanya walemae na kushindwa kufanya shughuli zao kwa ufanisi," anaelimisha.

Kasilda anataja madhara kama ya ulemavu, mabaka mwilini, kuvimba miguu, saratani za tumbo na kibofu cha mkojo, upofu wa macho na kwa mtoto kuwa dhaifu na maendeleo yao huwa hafifu shuleni. Pia familia inapokumbwa na madhara hayo, huathirika na hali ya kiuchumi kitaifa inayumba

**WADAU**

Subira Togorai, mkaziwa Mtaa wa Magomeni, Bagamoyo, anaishukuru Taasisi ya Afya Ifakara kwa kutoa elimu na hamasa kwa wananchi kumeza dawa, kwa sababu bado umma wao una uelewa mdogo kuhusu magonjwa hayo na athari zinazowanyemelea ya kuwadhuru.

"Ingawa IHI (Taasisi Ifakara) imekuwa ikijitahidi kutoa elimu kuhusu magonjwa haya hasa ngirimaji, kichocho na minyoo ya tumbo," anayesisitiza wakazi Bagamoyo kupewa kipaumbele katika tiba ya maradhi hayo, akiambatanisha na ombi la ziada:

"Serikali itusaidie kutatua tatizo la ugonjwa wa 'UTI' kwa sababu ugonjwa wa UTI unatusumbua sana wananchi wa Bagamoyo, ikiwamo watoto na hatufahamu unasababishwa na nini?"

Mtaalamu ardhi aliyeko Bagamoyo, Magdi Othman, ambaye shirika lake linashirikiana na wadau wengine wa afya, ikiwamo wizara mama, katika vita hiyo dhidi ya magonjwa yasiyo na kipaumbele yanatokomezwa kwenye jamii yao.

Othman anasema, kila mwaka taasisi anayotumikia hufanya mapitio katika mikoa mbalimbali, kuangalia watu wenye matatizo ya ugonjwa wa trakoma na kusimamia matibabu yao bure .

Anataja mikoa hiyo ni Dodoma, Pwani, Mtwara, Singida, Arusha na anafafanua: "Kila baada ya miezi sita, tunaenda tena kuwatembelea wale wagonjwa ambao tumewapatia matibabu, ili kuona wanaendeleaje na kama bado wana matatizo, tuweze kuwasaidia."

***Usikose makala nyingine Alhamis ijayo.***

## Serikali yazindua mwongozo matibabu ya saratani nchini



Tiba saratani inaendelea hospitalini Ocean Road.

**Na Yasmine Protace**

MWONGOZO wa aina yoyote, kila unapoanzishwa katika sehemu yoyote, huwa unasaidia kuleta mawasiliano mazuri ya kiutendaji katika kuleta mabadiliko katika sehemu husika.

Hivi karibuni, serikali nchini ilizindua mwongozo wa kitaifa wa tiba ya magonjwa ya saratani, utakaoziwezesha hospitali za serikali na binafsi kutoa matibabu sawa na kurahisisha mawasiliano, kati ya madaktari bingwa na wataalamu wengine.

Kuzinduliwa mwongozo huo, ni baada ya hospitali za kanda kuanza kutoa tiba za saratani, pia kuongezeka hospitali binafsi na za umma zinazotibu ugonjwa huo kwa nchini.

Ni hatua zaidi, kwani kwa kipindi kirefu hospitali nyingi nchini zimekuwa zikitumia miongozo tofauti na ile ya nje ya nchi kimataifa.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema huduma za saratani zinasambaa katika hospitali mbalimbali nchini, hivyo utoaji wake ni lazima ufanyike kwa kiwango kinachopaswa.

"Kutokana na kuanzishwa kwa mwongozo, hatua hiyo itarahisisha mawasiliano katika utoaji huduma za saratani," anasema.

Anafafanua kwamba, kuwapo miongozo tofauti kulisababisha kukoswekana usawa katika tiba za wagonjwa, pia changamoto ya mgonjwa kuendelea na tiba sahihi, anapopewa rufani ya kwenda hospitali nyingine.

"Kuwapo mwongozo huu kutawezesha kurahisisha mawasiliano kati ya madaktari bingwa na wataalamu wengine wa matibabu ya saratani, kote nchini kurahisisha uandaaji matokeo na ununuzi wa dawa na vitenganishi vinavyotumika katika matibabu ya saratani.

"Mwongozo huu pia umetoa orodha ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya matibabu ya saratani ambayo itatumika kama mwongozo kwa ajili ya manunuzi na matumizi nchini," amesema Ummy Mwalimu.

Amesema mwongozo huo pia utawezesha wananchi kupata huduma bora na za viwango vya juu katika vituo vyote vya matibabu kwa kuwa tiba zote zitapangwa kwa kufuata mwongozo huo.

Waziri Ummy amesema pia utawezesha kutoa mwongozo kwa mfuko wa taifa wa bima ya afya NHIF kuhusu dawa na vipimo mbalimbali stahiki kwa wagonjwa wa saratani.

"Mfuko wa Taifa NHIF uhakikishe unatumia mwongozo huu katika kuweka vitita vya huduma za saratani hapa nchini kwani katika ile standard treatment guideline kuna baadhi ya dawa za kutibu saratani hazikuorodheshwa, na niwaambie mmeweka masharti magumu sana katika vipimo hivi CT Scan na MRI nani anapima mara kwa mara tuondoe baadhi ya vikwazo na hili NHIF mkalitekeleze," ameagiza. Ameagiza mwongozo huo utumike na vituo vyote vinavyotoa tiba za saratani nchini;

"Ninafahamu hospitali zote zilishiriki kuuandaa hivyo sitegemei kusikia kuna hospitali inafanya tiba nje ya mwongozo huu, ninaagiza pia wizara kufanya mapitio ili kuhakikisha dawa zote zinazotibu saratani zinajumuishwa katika mwongozo huu."

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk Julius Mwaiselage amesema, matumizi ya mwongozo huo yamefanyiwa majaribio kwa kipindi cha miezi sita katika taasisi hii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha St Francisco."

***Soma zaidi saratani uk. 20***

AFYA

# RC Nchimbi anavyojipanga kijeshi katika lishe bora mkoa Singida

## •Viashiria vya wazi vyajionyesha
## •Mradi kimataifa wampigia makofi



Veronica Mussa, mkazi wa Singida akimnyonyesha mtoto katika namma sahihi inayoshauriwa kupitia mafunzo kutoka asasi ya Enrich.

Mkuu wa Mkoa Singida, Dk. Rehema Nchimbi. **PICHA: MAKTABA.**

**Na John Mapepele, Singida**

MAADHIMISHO ya siku ya Chakula Duniani, ni wito wa kutokomeza baa la njaa, kwa kujiwekea sera na mikakati ya kuwa na chakula chenye lishe bora, kinachopatikana wakati wote kwa bei nafuu na kwa watu wote.

Kimataifa, Siku ya Chakula Duniani, huadhimishwa kila Oktoba 16. Mwaka jana, kaulimbiu ilikuwa "Lishe Bora kwa Ulimwengu Usio na Njaa" ikilenga kuhamasisha jamii na wadau wa sekta ya kilimo kuhakikisha dunia inakuwa na chakula cha kutosha wakati wote na kwa watu wote.

Mwaka jana, kitaifa yalifanyika mkoani Singida huku Serikali ya Mkoa wa Singida na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alirejea takwimu za Wizara ya Kilimo kwamba, upatikanaji chakula kwa mwaka 2019/2020 ni nzuri.

Anasema, Tanzania ina chakula cha kutosha kujitosheleza kwa asilimia 119. Kwa maana hiyo, kuna ziada, uzalishaji mazao ya chakula ulifikia tani 16,408,309 ikilinganishWa na mahitaji ambayo ni tani 13,842,536. Kati ya hizo Tani 9,007, 909 ni mazao ya nafaka na tani 7,400,400 ni mazao yasiyo nafaka.

> **"Wanaotakiwa kupiga kelele kuhusu mazingira pia ni wataalam wa afya, lakini utashangaa mtu anakata miti na kuchoma mkaa kijijini, lakini muuguzi anamuangalia tu.**

**DHANA LISHE**

Dk. Nchimbi anasema upande wa Mkoa wa Singida, suala la lishe bora ni kipaumbele cha kwanza ambalo limewekewa mkakati madhubuti ili kuboresha afya za watoto na wananchi kwa ujumla.

Anasema, kutokana na suala hilo kuwa kipaumbele tayari ameweka utaratibu wa kusainiana mkataba kila mwaka na kila Mkuu wa Wilaya katika Mkoa wa Singida, baada ya kumaliza mwaka tathlmini inafanyika na hatua stahiki zinachukuliwa kulingana na hali ya utekelezaji.

"Lishe ni kila kitu kwetu, lishe ndiyo inatupa utambulisho wa taifa letu," anasema Mkuu wa Mkoa, huku akiwaelekeza watendaji wote wa kiserikali Singida kuwa wa kwanza kujitafakari kuhusu lishe, kabla ya kuwaambia wananchi.

Akipokea matokeo ya utafiti kuhusu uboreshaji wa huduma za lishe katika kuimarisha Afya ya Uzazi kwa Mama na Mtoto kwa Mkoa wa Singida na Shinyanga kwa miaka mitatu kuanzia 2016, uliofanywa na Shirika la World Vision, Dk NchimbI ana kauli ya ufafanuzi.

Mkuu wa Mkoa analieleza hilo linalipitia mradi wa Enrich akisema utafiti ni muhimu na wa lazima, kusaidia kutoa majibu sahihi na lazima zitunzwe lakini muhimu zaidi, ili kuwarudia wananchi ambao ndiyo walengwa wa kwanza.

"Wanaotakiwa kupiga kelele kuhusu mazingira pia ni wataalam wa afya, lakini utashangaa mtu anakata miti na kuchoma mkaa kijijini, lakini muuguzi anamuangalia tu.

"Hatuwezi kufika tunapotaka kufika kilishe kama hatutakemea uharibifu wa mazingira kwa kuwa hili ni suala mtambuka" anasisitiza Dk. Nchimbi

**KILICHOJIRI UTAFITI**

Kwa mujibu wa utafiti wa Enrich, kulikuwapo vipengele vitatu vilivyofanyiwa utafiti ambavyo ni afya na lishe, jinsia na uchechemuaji na kilimo kupitia viashiria mbalimbali.

Katika kipengele cha afya na lishe, ilibeba viashiria vinne ambapo katika kila kimoja, kimekuwa na mafanikio. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka ujao.

Akiwasilisha ripoti ya mafanikio katika kikao cha wadau wa mikoa ya Singida na Shinyanga, ambao Dk. Nchimbi alikuwa mgeni rasmi, Meneja Mradi Mwivano Malimbwi, anasema katika kiashiria cha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee, kumekuwapo ongezeko la asilimia 6.9, akirejea takwimu mwaka 2016 ilikuwa asilimia 69.3 na sasa imefikia asilimia 76.2.

Kwa kiashiria cha waliotumia kiwango cha chini cha lishe kilichokubalika kimepanda kutoka asilimia 16.7 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 17.9 mwaka 2020.

Pia, walengwa waliofika kliniki ya wajawazito iliongezeka kutoka asilimia 45 mwaka 2016 hadi asilimia 51.5 mwaka huu, ushuhuda wa matokeo makubwa zaidi ni kwenye kiashiria cha walengwa waliosaidiwa na mhudumu mwenye ujuzi wakati wa kujifungua, iliongezeka kwa asilimia 9.5; mwaka 2016 ilikuwa asilimia 74 na mwaka 2020 imefikia asilimia 83.5

Malimbwi amepongeza juhudi za Mkuu wa Mkoa wa Singida, katika kusimamia suala la lishe mkoani na mikakati anayotumia kufikia hatua hiyo tajwa, ikiendana na mafanikio yaliyopatikana katika mradi wa Enrich.

**VIKUNDI LISHE**

"Lazima niwe mkweli mama yetu Dk. Nchimbi, amekuwa akipiga kelele kila wakati kwa wananchi hususani wanawake badala ya kuchukua vipodozi kwenye mikoba tuchukue matunda kwa ajili ya watoto wetu, ndiyo maana tunamwita Mama Lishe", aliongeza Mwivano

Katika kipindi hiki wanakikundi lishe 918 wamepatiwa mafunzo ya mkoba wa siku 1000, masuala ya msingi ya lishe, mahitaji ya lishe ya mama na wanawake wajawazito ambapo wanaume ni 483 na wanawake ni 435.

"Tumejua kuna vyakula bora vingi katika kijiji chetu na tumejifunza jinsi ya kuandaa mlo bora kulingana na makundi ya vyakula ili kupata virutubisho muhimu" anasema Grace Msengi, Katibu wa Kikundi Lishe Kijiji cha Mkwese.

Katika kiashiria cha uwezeshaji wanawake kiuchumi, kulikuwapo asilimia 34.2 mwaka 2016 sasa imefika asilimia 39.

INAENDELEA UK.19

AFYA

# RC Nchimbi anavyojipanga kijeshi katika lishe bora mkoa Singida



Samia Mkumbo, akimlisha mwanawe mlo unaozingatia usahihi wa virutubisho vyenye mchanganyiko nimuhimu.

INATOKA UK.18

Usawa wa kijinsia katika utoaji huduma za afya mwaka 2016, ilikuwa asilimia 60 na mwaka huu imefika asilimia 76 na idadi ya vituo vinavyotoa huduma za afya vinavyotekeleza sera/mpango wa lishe wa taifa, vilikuwa asilimia 12 mwaka 2016 na sasa vimefika asilimia 16.

Mkurugenzi wa Jukwaa la Lishe nchini, Tumaini Mikindo, anasema hivi sasa nchi imepiga hatua kwa asilimia 10 katika upunguzaji udumavu, kuanzi mwaka 2010 ilikuwa asilimia 42 na mwaka 2018 ikafikia asilimia 32.

Anasema, kwa sasa uelewa umeongezeka kutokana na juhudi za serikali kuweka mifumo bora inayowashirikisha wadau katika kutekeleza sera ya chakula na lishe kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa.

"Katika mkoa wetu hali ya udumavu imeendelea kupungua kutoka asilimia 39 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 29 mwaka 2018 wakati hali ya ukondefu ilikuwa asilimia 9 mwaka 2010 na kupungua hadi asilimia 5 mwaka 2018 "anaongeza Teda Sinde, Ofisa Lishe Mkoa Singida

Anaishauri umefika wakati jamii iachane na mila potofu katika ulishaji na kunyonyeshaji, badala yake wazingatie kanuni bora za kulishaji na kunyonyesha watoto wachanga.

**KILIMO KILIVYO**

Katika kipengele cha Kilimo, kunatajwa kuwapo viashiria vitatu vyenye mafanikio, kwanza ni kilimo katika mikoa hiyo katika kipindi hicho mazao yanayorutubishwa kibaiolojia mwaka 2016 ilikuwa asilimia 9.1 na kukua hadi asilimia 30.2 ya sasa.

Kiwango cha kiashiria cha uanzishaji bustani wa mboga nyumbani ulianza kwa asilimia 8.9 na sasa iko katika asilimia 26.

Kiashiria cha mwisho kuhusu elimu juu ya viazi vitamu vya lishe mwaka 2016 ni asilimia 0.5 ambapo ilikuwa na kufikia asilimia 5.4 mwaka 2020.

**TAARIFA FAO**

Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo dunia (FAO) zinaonesha kila mwaka kuna theluthi moja ya chakula kinachozalishwa kwa ajili ya binadamu kinapotea au kutupwa kama taka, wakati kuna watu milioni 820 duniani, wanaoendelea kupekenywa kwa baa la njaa na utapiamlo wa kutisha.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Angelina Lutambi, anasema kuna hoja ya kujenga utamaduni wa matumizi bora ya chakula, kulinda na kutunza mazingira nyumba ya wote.

Mwaka ujao inatarajiwa Jumuiya ya Kimataifa itakuwa na kongamano la kimataifa kuhusu mifumo ya chakula, ikiwa ni sehemu ya mchakato wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Binadamu ifikapo mwaka 2030.

Dk. Angelina anatoa wito kila sekta mtambuka kama kilimo na maji kupanga nafasi ya lishe, aliyosisitiza kuwa mkakati wa mkoa ni kushirikiana na wadau katika kuboresha huduma za kishe katika kuimarisha afya ya uzazi kwa mama na mtoto.

Dk. Angelina anasema, wadau wa afya wamekuwa wengi na kila mmoja anaandaa programu za afya bila ya kuangalia, imeamua kuwakutanisha ili kujua namna bora ya kufanya shughuli hizo kwa manufaa ya taifa.

Anasema mpango huo ni nyenzo inayotumiwa na timu ya uendeshaji afya kimkoa katika kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini shughuli mbalimbali za afya, ustawi wa jamii na lishe katika halmashauri, vituo vya kutoa huduma za afya na katika ngazi ya Jamii, kila mwaka.

> **"Lazima niwe mkweli mama yetu Dk. Nchimbi, amekuwa akipiga kelele kila wakati kwa wananchi hususani wanawake badala ya kuchukua vipodozi kwenye mikoba tuchukue matunda kwa ajili ya watoto wetu, ndiyo maana tunamwita Mama Lishe", aliongeza Mwivano**



Wanawake wakiwa katika shamba la viazi vitamu, katika kijiji cha Iglansoni Singida. **PICHA ZOTE: JOHN MAPEPELE.**

AFYA

SIKU YA SARATANI

# Bosi Ocean Road aorodhesha aina 10 vinara kuitesa nchi

- Shingo ya kizazi, matiti ziko juu
- Ina yanaiyojificha nje ya mazoea

Na Sabato Kasika

NI siku mbili zimepita tangu kilele cha maadhimishio ya Siku ya Saratani Duniani. Bado taarifa zinaanika namna shingo ya kizazi inavyotajwa kuongoza kuwa na wagonjwa wengi nchini kuliko saratani nyingine.

Jiji la Dar es Salaam lenye wakazi wengi kitaifa linaongoza kwa saratani ya matiti inayochangia kuwafanya kinamama wengi kuzaa watoto wachache.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage, anataja saratani nyingine 10 zinazowasumbua Watanzania ni ya koo, ngozi, matezi, damu, kibofu cha mkojo na tezi dume.

Anafafanua kwamba kuna aina 200 za saratani duniani, lakini Tanzania zipo 10 ambazo zinaongoza, huku ya shingo la kizazi na matiti zikiwa juu na kuongezeka.

Mkurugenzi huyo anataja chanzo kikuu cha saratani zote, ni mlo usiozingatia kanuni na kwamba kila mwaka, taasisi hiyo inapata wagonjwa wapya 7,600.

"Asilimia 14 ya wagonjwa hao ni wa saratani ya matiti, hivyo ni muhimu watu kufuata kanuni bora za lishe na kuzaa watoto wa kutosha na kuwanyonyesha kwa muda ulioshauriwa kitaalamu," anasema Dk. Mwaiselage.

Inaelezwa walio katika hatari kubwa ya saratani ni wavutaji wa sigara na wanywaji wa pombe, hivyo wenye tabia ya kupenda kutumia vilevi hivyo wanashauriwa kuachana navyo.

Aidha, theluthi moja ya waliofariki kwa ugonjwa wa saratani mwaka jana, sababu kuwa ilikuwa vilevi hiyo pamoja na uzito mkubwa wa mwili, matumizi na kutofanya mazoezi.

**JICHO LA WHO**

Kwa mujibu wa WHO, tahadhari ni kwamba kuna hatari dunia kushuhudia ongezeko la asilimia 60 la hatari ya saratani katika miongo miwili ijayo. Nchi maskini ndizo zilizoko katika hatari hiyo kwa zaidi ya asilimia 80.

WHO inafafanua sababu ni kuwekezwa rasilimali kidogo za kiafya katika kupambana na magonjwa ya kuambukiza na kuimarisha afya ya mama na mtoto, hali inayofanya kati huduma za afya kukosa vifaa vya kuzuia, kugundua na kutibu saratani.

Inafafanua kuwa mwaka jana, zaidi ya asilimia 90 ya nchi zenye kipato cha juu ziliripoti kuwa na huduma kamili za matibabu ya saratani, zinazopatikana katika mfumo wa afya ya umma, ikilinganishwa na chini ya asilimia 15 katika nchi zenye kipato cha chini.




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk Julius Mwaiselage.

> "Asilimia 14 ya wagonjwa hao ni wa saratani ya matiti, hivyo ni muhimu watu kufuata kanuni bora za lishe na kuzaa watoto wa kutosha na kuwanyonyesha kwa muda ulioshauriwa kitaalamu," anasema Dk. Mwaiselage.

Mkurugenzi Mkuu Msaidizi wa Huduma ya Afya kwa Wote na magonjwa Yanayoambukizwa na yasiyoambukiza wa WHO, Dk. Ren Minghui, anashauri umuhimu wa kushughulikia tofauti za usawa kati ya huduma za saratani, kati ya nchi tajiri na maskini.

Dk. Minghui anasema, iwapo watu wanapata huduma za msingi na mifumo ya uhamishaji, saratani inaweza kugundulika mapema, kutibiwa vizuri na kupona na kwamba ugonjwa huo haupaswi kuwa katika sura ya 'adhabu ya kifo' kwa yeyote na kila mahali.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk Tedros Adhanom Ghebreyesus, anasema kulikuwapo uwezekano maisha ya watu milioni saba yangeokolewa katika kipindi cha muongo mmoja ujao.

Dk. Ghebreyesus anasema ni muhimu kutambua sayansi inayofaa kwa hali ya kila nchi, kwa kushugulikia saratani kupitia mifumo ya afya ya umma kwa wote na kwa kuhamasisha wadau mbalimbali kufanya kazi kwa pamoja.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani Ocean Road pamoja na wadau mbalimbali huadhimisha siku ya saratani kwa kutoa elimu ya umuhimu wa kuzuia na kujikinga na madharai yatokanayo na kansa.

Jinsia zote zinasubuliwa na saratani za ngozi na koo, huku kinababa peke yao wanasumbuliwa zaidi na saratani za tezi dume na tezi; kinanamama wao tabu yao kipekee ni katika saratani za shingo ya kizazi na matiti.



Mgonjwa wa kansa ya titi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MZIZI WAKE**

Kwa mujibu wa taarifa za kiafya, saratani duniani vyanzo vyake vimegawanyika katika sehemu tatu: Virusi vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi; bakteria wasababishao saratani ya tumbo; na vimelea vya kichocho kwa saratani ya kibofu cha mkojo.

Pia, katika mfumo wa maisha, uvutaji wa sigara, kula mlo usio kamili na vyenye mafuta kwa wingi, kutokula matunda na mboga, unywaji pombe kupita kiasi, ulaji sukari kwa ziada na matumizi ya dawa za kulevya na kutokufanya mazoezi, kunachangia.'

Pia, kuna vyanzo vya uzito na unene uliopitliza, mtu, kutofanya mazoezi, sambamba na vyanzo kama mionzi ya miale ya jua inayoathiri ngozi, hasa kwa walemavu wa ngozi, urithi katika familia, eneo la mfano ni katika saratani za matiti na utumbo.

Inaelezwa, saratani ni ugonjwa unaochukua muda mrefu kujitokeza, hata wastani kati ya miaka 10 hadi 20, hivyo kuna wakati inakuwa vigumu kugundua chanzo chake.



# Mpango maalum upandaji miti waja

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

OFISI ya misitu Mkoa wa Mbeya imeanzisha mpango maalum wa upandaji wa miti kwa kuhusisha taasisi mbalimbali zikiwamo shule na madhehebu ya dini kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa karibu wa miche iliyopandwa.

Kauli hiyo imetolewa jana na Ofisa Misitu Mkoa wa Mbeya, Simon Parmet, wakati wakizungumza na gazeti hili na kuwa mpango huo umekuwa na manufaa kutokana na jamii yenyewe kushiriki katika kutunza miche iliyopandwa katika maeneo mbalimbali.

Alisema mpango huo umekuwa na mwitikio mkubwa kutoka kwenye taasisi mbalimbali kwa mkoa wa Mbeya hususan maeneo ya shule, makanisa na misikiti na kuwa tangu kuanzishwa kwa mpango huo kumekuwa na mafanikio makubwa.

"Unajua tumeamua kuzishirikisha taasisi kwa lengo la kujenga uelewa katika jamii juu ya umuhimu wa kupanda miti kwa lengo la kutunza mazingira katika jamii," alisema Parmet.

Alisema miongoni mwa shule walizopanda miche hiyo ni Shule ya Msingi Kimbila wilayani Rungwem na kuwa mpango huo umeiwezesha jamii wakiwamo wanafunzi kushiriki moja kwa moja kusimamia na kutunza miche ya miti. Parmet alisema sehemu kubwa ya misitu kwa mkoa wa Mbeya ni kwa ajili ya hifadhi na kuwa kuna misitu ambayo inasimamiwa na serikali kuu ikiwamo misitu ya Kawetele na Kiwira, na kuwa kuna misitu ambayo inapandwa na watu binafsi kwa ajili ya biashara na inayopandwa ngazi za halmashauri.

Alisema kwa mkoa wa Mbeya umekuwa na hamasa kubwa ya upandaji wa misitu ikiwamo ya asili na ile isiyo kuwa ya asili kwa ajili ya kuhifadhi mazingira ngazi mbalimbali zikiwamo halmashauri na mtu mmoja mmoja, na kuwa mafanikio ya upandaji miti kunatokana na hali nzuri ya hewa na mvua za kutosha.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2018/19, jumla ya miti milioni 6,939,977 ilipandwa Mkoa wa Mbeya na kutolewa mfano kuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipanda miche 600,349 na Halmashauri ya Rungwe miche 1,889,295.

Alisema katika halmashsuri zote za mkoa hakuna misitu ya kuvuna isipokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pekee kwa ajili ya uvunaji wa mkaa na mbao na kwamba uvunaji huo umekuwa ukifanywa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyunga jijini Mbeya, Abdul Kisukari (kulia), akipokea msaada wa mifuko 100 ya saruji kutoka kwa Meneja Rasilimali Watu wa kampuni ya Tanzania Breweries Limited, Prudence Gerald (wa pili kutoka kulia), kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iyunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaotembea na majina ya wagombea CCM waonywa

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Chunya, Raphael Ilomo, amewaonya wanachama wa chama hicho kuacha kutembea na majina ya watu wanaokusudia kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Angalizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya sherehe za miaka 43 ya kuzaliwa kwa CCM ambayo yameazimishwa na jumuiya hiyo wilayani Chunya na kufanyika Kata ya Chalangwa.

Alisema kumekuwapo na baadhi ya wanachama katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na rais kuwapigia debe baadhi ya makada wanaotaka kugombea na kuwa vitendo hivyo havikubaliki kwa mujibu wa misingi na taratibu za chama hicho.

Ilomo alisema hali ya umoja na utulivu uliopo nchini umetokana na misingi mizuri iliyowekwa na usimamiwa na viongozi wa vyama vya Tanu na ASP na baadaye CCM, na kuwa wanachama wengine hawanabudi kuzingatia hilo katika kudumisha amani na umoja wa taifa hili.

Alisema CCM chini ya mwenyekiti wake, Rais John Magufuli imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi ikiwamo ya elimu, afya na miundombinu na kuwa wanachama wa CCM hawanabudi kujivunia maendeleo hayo.

"Uwezo aliouonyesha Rais katika kutekeleza Ilani ya CCM ni wazi kuwa kila Mtanzania anaona na kuwa kuna miradi mingi ikiwamo ya ujenzi wa shule, hospitali madaraja na mingine mingi, hivyo uchaguzi ujao itakuwa rahisi kwa CCM kushinda kutokana na kazi kubwa iliyofanywa.

Kwa upande wake mgeni rasmi, Petro Saka, Diwani wa Chalangwa, aliishauri CCM kuhakikisha inaisimamia serikali ili kutekeleza ilani na kuwa mpaka sasa kuna mafanikio makubwa.

# RC Chalamila aomba TRA

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetakiwa kufanya mapitio ya mkataba na kampuni zilizopewa dhamana ya kusambaza na kuuza mashine za kielektroniki za EFD kutokana na ufanisi mbovu wa mawakala hao katika kuwahudumia wateja.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyekuwa mgeni rasmi katika kikao cha wafanyabiashara mkoa wa Mbeya ambacho kiliitishwa na Kamisha Mkuu wa TRA kwa lengo la kutoa elimu wa wafanyabiashara kuhusiana na aina mbalimbali za kodi.

Alisema mawakala wengi wamekuwa ni wababaishaji na kuna uwezekano mkubwa wakawa wanakwamisha jitihada za TRA na serikali kwa ujumla za kuhakikisha wafanyabiashara wanaokidhi vigezo vya kuwa na mashine hizo wanazipata kwa wakati.

Chalamila alisema kwa mkoa wa Mbeya pekee amekutana na malalamiko ya wafanyabiashara ambao walikuwa wamelipia fedha kwa lengo la kupata mashine za kielektroniki (EFD), lakini wamekuwa wakizungushwa na mawakala hao kwa muda mrefu bila ya kupewa mashine hizo.

Alisema mwishoni mwa mwaka jana, alilazimika kuwatia ndani mawakala watatu wa mashine hizo kutokana na kubainika kuwa walikuwa wamechukua fedha za wafanyabiashara bila ya kuwapa mashine za EFD.

"Ndugu kamishna mimi kama mkuu wa mkoa niliwahi kukumbana na changamoto ya mmoja wa mawakala ambaye nilikuwa nimemlipa fedha zangu ili kupewa mashine ya EFD, lakini jambo la kushangaza hata mimi nilizungushwa kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu hadi meneja wa TRA mkoa wa Iringa alipoingilia kati," alisema Chalamila.

Pia mkuu huyo wa mkoa alitoa onyo kwa wafanyabiashara hao kuacha ujanja ujanja katika mchakato wa kufanya biashara na kuwa maendeleo ya nchi yoyote duniani yanategemea kodi na kuwa ni lazima kila mwananchi alipe kodi.



## HABARI DODOMA

# NEC yatoa neno kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imewataka wakazi wa Jiji la Dodoma kutumia maonyesho ya Wiki ya Sheria kujifunza sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi wakati wa kuelekea katika maandalizi ya uchaguzi mkuu 2020, ili kujua haki zao za msingi.

Rai hiyo ilitolewa na Ofisa Habari Mwandamizi wa NEC, Magreth Chambiri, katika mwendelezo wa Wiki ya Sheria hapa nchini, unaoendelea katika maeneo mbalimbali.

Chambiri alisema taifa linatarajia kuingia katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, ubunge na udiwani Oktoba mwaka huu, hivyo ni vema wananchi wakapata elimu ya kutosha kuhusiana na sheria ambayo itawasaidia kuwajenga ili wasidanganywe wakati wa uchaguzi.

Chambiri alisema NEC imeshiriki katika Wiki ya Sheria kwa kuwa uchaguzi mkuu unaendeshwa kwa sheria, taratibu na kanuni hivyo mwananchi anatakiwa azifahamu ili aweze kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo.

"Kama mnavyojua Tanzania inaelekea katika uchaguzi mkuu wa viongozi wa nchi mwaka huu, hivyo ni lazima Tume tutumie fursa hii kutoa elimu kwa wananchi," alisema Chambiri.

Aidha, Chambiri alisema NEC ndio ina jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, lengo likiwa kila Mtanzania aweze kupata elimu hiyo ili aweze kushiriki kikamilifu uchaguzi huo.

Chambiri amewataka wakazi wa Dodoma na mikoa ya jirani kwenda kwa wingi katika maonyesho hayo ili waweze kupata elimu itakayowasaidia katika shughuli zao mbalimbali zikiwamo za kisheria. Alisema kuwa wananchi wakijua sheria, taratibu na kanuni za uchaguzi, itasaidia uchaguzi wote kufanyika kwa haki, amani na usalama.

"Wakati mwingine nchi inaingia katika machafuko, kutokana na wananchi wake kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na uchaguzi," alisema. Chambiri.

Wakati huo huo, Chambiri alisema NEC inaendelea na zoezi la uandikishaji katika daftari la kudumu la mpigakura, ambapo kwa sasa wako Mkoa wa Morogoro.

Chambiri alisema baada ya kutoka Morogoro wataenda Mkoa wa Pwani, halafu watamalizia Dar es Salaam, na baadaye watatoa daftari hilo kwa ajili ya wananchi



Waliokuwa wajumbe wa kamati ya utekelezaji wa makubaliano yaliyosainiwa Oktoba 2019 kati ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kampuni ya Rom Solutions Co. Ltd, (kutoka kulia), ni Kamishna wa jeshi hilo, Mbaraka Semwanza, Naibu Kamishna Fikiri Salla, Naibu Kamishna Lesekelo Chaula, Naibu Kamishna Ully Mburuko, Mchumi wa jeshi hilo, Bonifance Kipomela na Mchumi Felis Mshana, wakisubiri kuhojiwa katika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jaji afunguka kuhusu jukumu utunzaji majengo ya mahakama

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma, Mustapha, Siyani, amesema jukumu la kuboresha na kutunza majengo ya mahakama si la mahakama pekee yake bali ni la kila mwananchi.

Akizungumza baada ya kuzindua jengo la Mahakama ya Mwanzo Bereko lililopo wilayani Kondoa mkoani Dodoma, Jaji Mfawidhi alisema watumishi wa mahakama pamoja na wananchi wa maeneo hayo hawanabudi kulinda miundombinu mizuri iliyopo kwa kuwa jukumu hilo ni la wananchi wote.

Alisema mahakama bado inayo kazi kubwa kwa kuwa mahakama za mwanzo nyingine zilizopo katika Wilaya ya Kondoa bado zinaendelea kufanyia kazi kwenye majengo chakavu na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa lengo zima la utoaji haki kwa wakati.

"Ufunguzi wa jengo hili ni sehemu tu ya safari ya maboresho ambayo Mahakama ya Tanzania imeamua kwa dhati kuifanya kwa kujenga na kukarabati miundombinu yake," alisema Jaji Mfawidhi Siyani.

Alisisitiza umuhimu wa kutunza jengo jipya alilozindua pamoja na kulinda samani zake kwani pasipo kufanya hivyo juhudi za Mahakama zitarudi nyumba.

Jaji Siyani ametoa rai kwa watumishi na wananchi wote kwa ujumla kuhakikisha wanalitunza jengo la Mahakama ya Mwanzo ili lidumu kwa muda mrefu zaidi.

Mbali na hilo alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuendelea kuweka misingi mizuri inayoiwezesha mahakama kufanya kazi za utoaji haki kama inavyotarajiwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa, Andrew Ng'hwani, alisema serikali itatoa ushirikiano kwa mahakama ili wananchi waweze kupata haki na kutumia miundombinu ya majengo ipasavyo.

"Hatutarajii wananchi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa sehemu ya kupata haki sasa ipo," alisema Ng'wani.

Alisema serikali pia itaweka mazingira yaliyo bora ili kuhakikisha mahakimu na wote wanaotoa haki wanafanya kazi katika mazingira yaliyo bora na hakwamishwi wanapotekeleza majukumu yao.

# Wataka gharama uchaguzi kupungua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANANCHI wameitaka serikali kuunganisha uchaguzi wote ili kupunguza gharama za uchaguzi ambazo hufanyika mara mbili kila baada ya miaka mitano.

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wananchi, Edward Rosikazoni, aliyetembea katika banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika Wiki ya Sheria inayoendela jijini hapa, alisema kuwa serikali inatakiwa kuangalia suala hilo kwa kuwa gharama za uchaguzi ni kubwa.

Edward alisema kuwa vitu ambavyo vimekuwa vikiwapa sintofahamu wananchi ni kuhusu kutoelewa uchaguzi mkubwa na mdogo unaofanyika kwa kipindi gani.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu uunganishwe uwe pamoja ili kuondoka sitofahamu kwa wananchi na kupunguza gharama kwa serikali," alisema Edward.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi kutoka tume hiyo, Dk. Cosmas Mwaisobwa, alisema wananchi wanatakiwa kufahamu uchaguzi mkubwa na mdogo ni mamlaka mbili tofauti na haviingiliani.

Aidha, alisema kuwa kwa sasa tume ya taifa ya uchaguzi ipo kwenye maandalizi ya uboreshaji wa daftari la mpigakura ambapo wanaotakiwa kushiriki katika zoezi hili ni wale ambao wamefikisha umri wa miaka 18, walihama sehemu moja kwenda nyingine, na waliopoteza kadi za mpigakura.

"Baada ya hapo sasa ndipo litatengenezwa sasa daftari rasmi la mpigakura wananchi watatakiwa waende wakapate rasmi haki yao ya mpigakura," alisema Mwaisobwa.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa mpaka sasa wamefikia mikoa 28, ya uboreshaji wa daftari la kudumu la mpigakura Tanzania Bara na visiwani, ambapo kwa sasa zoezi linaendelea katika mkoa wa Morogoro na baaada ya hapo litaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani Februari 10 mpaka 16, mwaka huu.

Alitoa wito kwa wananchi kutumia nafasi hiyo muhimu kushiriki katika zoezi nzima la kujiandikisha ili kuchagua viongozi bora, ambao watakaowaletea maendeleo katika maeneo yao.



## ‘Hakuna Mzanzibari aliyepata corona’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UBALOZI wa mdogo wa China uliopo Zanzibar, umesema hakuna Mzanzibari yeyote aliyeathirika na virusi vya corona.

Hayo yameelezwa jana na Balozi Mdogo wa China Zanzibar, Xie Xiawu, wakati akizungumza waandishi wa habari kuhusiana na virusi hivyo.

Alisema nchini China kuna Watanzania 4,000 kati ya hao 400 ni wanafunzi na wote wapo salama.

“Wazee wasiwe na hofu kwa watoto wao hadi sasa hakuna Mtanzania yeyote aliyepata maradhi hayo na wako salama na kwamba Serikali ya China inawaangalia kwa umakini,” alisema Balozi huyo.

Alisema hawapendi kuona maradhi hayo yanaendelea kuathiri wananchi wengine, na kwamba ikitokea Mtanzania ameathirika atatibiwa kwa ustadi mkubwa ili kuokoa maisha yake.

Aidha, alisema serikali yao iko makini na maradhi hayo ili yasiendelee kusambaa maeneo mengine na kwamba serikali itajenga hospitali kubwa kwa muda wa siku kumi na kuwapeleka waathirika wa maradhi hayo na kuwahudumia kwa matibabu ya hali ya juu.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Dk. Juma Muhamed Salum, alitaka waandishi wa habari kuandika habari kwa kuondoa maumivu ya wale walio athiriwa na maradhi hayo nasiyo kushabikia bila ya kueleza ukweli.

Alieleza kuwa waandishi waunge mkono kupiga vita maradhi hayo mabaya ambayo madaktari bingwa wamo kuyapatia ufumbuzi kuyashinda.

Mkurugenzi huyo alipongeza ubalozi huo kwa kuwatoa hofu Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla kwa kusema China iko wazi katika majibu ya mambo yake kwa kutekeleza kwa vitendo kauli zake za uhakika.

# SMZ yajipanga kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma N’hunga, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo kutengeneza maeneo yaliyoathiriwa.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya, aliyetaka kujua mpango wa serikali kuzuwia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Alisema kuwa miongoni mwa hatua hizo zinazochukuliwa ni kupanda miti ya aina ya mikoko, mikandaa na kujenga matuta na kuta maalum kwa baadhi ya maeneo ili kuzuia uingiaji maji ya bahari.

Aidha, alisema serikali imekua ikielimisha jamii na kukusanya taarifa za kina za maeneo mbalimbali yaliyoathirika na hali hiyo kwa kuweka kwenye mfumo wa ramani.

“Ramani ya visiwa vya Zanzibar ya mwaka 1984 iliyochorwa na wataalamu kutoka Uingereza kwa kushirikiana na wataalamu wa Zanzibar inaonyesha kwamba Zanzibar ina ukubwa wa kilomita za mraba 2,654,” alisema na kuongeza: “Serikali ya Zanzibar haijatoa ramani rasmi yenye kuonyesha ukubwa wa visiwa vya Zanzibar ingawa serikali inaamini kuwa kuna maeneo yameongezeka na mengine yamepungua.”

Alisema kuwa utafiti mbalimbali umefanyika kujua ukubwa wa baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mmomonyoko wa fukwe. Kwa mujibu wa mwakilishi huyo, hakuna utafiti uliyofanywa kwa Zanzibar nzima ya kujua kilomita ngapi za mraba zilizoathiriwa na mmomonyoko huo.



Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya (wa pili kushoto), akizungumza na wajumbe wenzake nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Z’bar yajigamba kwa wataalamu Kiswahili

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ZANZIBAR ina wataalamu wa kutosha ambao wanaweza kuwa walimu wa kufundisha Kiswahili katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na nje ya jumuiya hiyo, imeelezwa.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Gavu, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Katika swali lake la msingi Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya Haji, aliyetaka kujua Zanzibar inawataalamu wangapi wa Kiswahili ambao wanaweza kuwa walimu wa kufundisha Kiswahili nchi za SADC na nje ya SADC.

Waziri Gavu alisema ili uwe mwalimu mzuri wa kufundisha lugha ni vyema kuwa na uwezo wa kuzifahamu zaidi ya lugha iliyo na kuwa na utaalamu nayo.

Alieleza kuwa serikali kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Suza) imeanzisha utaratibu wa kusaidia lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli mbalimbali. Alisema kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa Kiswahili kila siku pamoja na wageni kutoka nchi mbalimbali duniani wanaofika Zanzibar kujifunza lugha hiyo.

Alisema nchi hizo ni pamoja na Rwanda, Uganda, Burundi na Sudan Kusini ambapo maofisa mbalimbali kutoka nchi hizo wamebainisha kuwa Kiswahili ni lugha rasilimali kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Alisema kwa upande wa Sudan Kusini wamefikia hatua ya kutaka Kiswahili kifundishwe katika ngazi mbalimbali za elimu kuanzia na elimu ya msingi.

# Ma-DC, DAS wapewa somo utendaji haki

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WAKUU wa Wilaya na Makatibu Tawala wameshauriwa kuwa karibu na shughuli za mahakama ili kuhakikisha ikitenda haki pasipo kumwonea mwananchi, huku wakitakiwa kutengeneza mfumo wa masikilizano na kutoingilia mfumo wa kisheria ili kuleta utulivu na ushamilishaji wa utendaji haki.

Akizungumza katika kikao kazi cha pamoja kilichowakutanisha Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala pamoja na Watendaji wa Mahakama kujadili muundo na utendaji kazi wa kamati za maadili za mahakimu wa mikoa na wilaya, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema ofisi ya mkuu wa wilaya haikatazwi kutengeneza mifumo ya mawasiliano na siyo kuingilia mifumo ya kisheria, lakini mifumo ambayo italeta utulivu itashamilisha utoaji wa haki bila kuathiri nafasi ya kila mhimili.

Aliongeza kuwa mahakama nayo itahitaji mifumo mingine kwenye utekelezaji wa maelekezo yake hivyo cha msingi ni kuaminiana ili watu wote watambue na kuamini kile kinachofanywa na mahakama kuwa ni haki.

kwa upande wake Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, Joachim Tiganga, ameagiza mahakimu kufanya kazi kwa uzalendo na uadilifu bila kwenda kinyume cha taratibu za kisheria na maadili ya kazi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu kwa uharaka na usawa.

Alisema kila hakimu ni kiongozi kwa mujibu wa sheria, hivyo jukumu lake ni kuhakikisha watu wote wanaofanya kazi chini yake na kutekeleza maadili kama ambavyo sheria inavyowataka.

"Ikitokea mtumishi yoyote anayefanya kinyume cha maadili na asichukue hatua anachukuliwa na yeye kuwa amekubaliana na uovu uliofanyika na yeye anaweza kuchukuliwa hatua kama kosa la kimaadili," alisema Tiganga.

Akizumgumza kwa niaba ya wenzake Mkuu wa Wilaya ya Magu, Philemon Sengati, alisema watahakikisha wanayafanyia kazi maagizo yote waliopatiwa kwa uweledi zaidi na kuhakikisha watumishi wa mahakama wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria taratibu na maadili ya utumishi wa umma.

"Sisi kama viongozi na wenyeviti wa hizo kamati tutahakikisha baada ya hii semina tutaenda kuwahamasisha watumishi wetu kufanya kazi kwa nidhamu na weledi mkubwa katika kuwatendea haki wananchi," alisema Sengati.



Mwendesha guta akimkokota mwenzake kwa staili ambayo ni hatari kwa usalama barabarani, baada ya kupata pancha katika eneo la Magomeni Mwembechai, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shinyanga yapungukiwa madarasa 508

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MANISPAA ya Shinyanga inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 508 katika shule za msingi na sekondari kutokana na kuwapo na idadi kubwa ya wanafunzi, na kusababisha mrundikano darasani.

Hali hiyo inasababisha wanafunzi wengine wakisomea chini ya miti. Hayo yalibainishwa juzi kwenye kikao cha bajeti cha baraza la madiwani Manispaa ya Shinyanga na maofisa elimu msingi na sekondari, kuwa madiwani wanatakiwa wahamasishe wananchi kuanzisha ujenzi wa maboma, ambapo serikali itayamalizia, ili kupunguza upungufu wa vyumba vya madarasa. Akizungumza kwenye baraza hilo, Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, alisema wanakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 439, ambapo mahitaji ni 975, na vilivyopo ni 939 na kusababisha mrundikano wa wanafunzi darasani na wengine kusomea chini ya miti.

Naye Ofisa Elimu wa Shule za Sekondari Manispaa hiyo, Lucas Mzungu, alisema wanakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 69, mahitaji ni 270, na vilivyopo ni 201, na kufanya jumla ya upungufu wa vyumba hivyo kwa manispaa yote kwa shule za msingi na sekondari kuwa 508.

"Kutokana na upungufu huu, huku bajeti yetu ikiwa ni ndogo na haiwezi kujenga vyumba vyote hivi vya madarasa, napenda kuwaomba madiwani wakahamasishe wananchi kuanzisha ujenzi wa maboma ya madarasa, ambapo serikali itayamalizia ili kupunguza upungufu uliopo," alisema Mkanga.

Diwani wa Mwamalili, Paulo Machela, alielezea kusikitishwa na taarifa ya upungufu wa vyumba vya madarasa na kubainisha yale madarasa mawili ambayo yapo kwenye bajeti katika Shule ya Msingi Ndala 'B' na Azimio ya jengwe hadi yakamilike, huku utaratibu mwingine ukiandaliwa wa kujengwa madarasa mengine.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwasisitiza madiwani kwenda kuhamasisha wananchi kuchangia shughuli za maendeleo, ikiwamo uanzishwaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa na kuongeza kuwa elimu ya bila malipo inazuia wananchi kuchangia maendeleo.

# Mikopo mikubwa ya muda mrefu yaja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya DCB imesema sasa inao mtaji wa kutosha katika kutoa mikopo mikubwa zaidi na ya muda mrefu kwa wateja wake baada ya kupata faida mfululizo, hivyo kujiimarisha kibiashara.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Fedha wa DCB, Zacharia Kapama, sambamba na mafanikio ya kifedha ya benki hiyo iliyoyapata kwa mwaka 2019.

Kapama alisema mwaka 2008, benki ilifanya vizuri katika miaka yote tokea iliponzishwa Septemba 2001.

"Pamoja na uwezo wetu wa kutoa mikopo mikubwa ya muda mrefu kunakochagizwa na utendaji wetu bora wa kifedha unatokana na faida ya Sh. bilioni 2.3 kwa mwaka jana, ukilinganisha na Sh. bilioni 1.6 tuliyoipata mwaka 2018, DCB imefanikiwa kuzindua mfumo wa akaunti za kidijitali ambapo umeiwezesha kuhudumia wateja wengi zaidi na kuwafikia hadi wale wa vijijini hivyo kuongeza ukuaji wa mapato na ongezeko la idadi ya wateja na ufanisi katika utoaji huduma," alisema Kapama.

Naye Mkurugenzi wa Biashara, James Ngaluko, alisema benki imeendelea kuingiza huduma na bidhaa mpya sokoni zinazokidhi mahitaji ya kibenki ya wateja wao.

"Mafanikio ya benki yetu yanaendana na bidhaa bora na za kiubunifu tunazoziingiza sokoni, tumefanikiwa kuzindua huduma na bidhaa mpya kwa wateja wetu ambazo ni Lamba kwanza (Fixed deposit), Akaunti ya Skonga, DCB Sokoni, pamoja na garantii za makandarasi zisizo na dhamana wakati wa kuomba tenda.

"Tumeboresha huduma ya mikopo ya ujenzi wa nyumba kwa kuongeza ushirikiano na Kampuni ya Mikopo Tanzania (TMRC), pia benki imeboresha gharama kwa kuondoa gharama katika akaunti za community kama vikoba, akaunti za miradi ya serikali, na akaunti za wastaafu, hii imepelekea kuongeza idadi kubwa ya wateja ambao wengi ni wa kipato cha cha chini na cha kati," aliongeza Bwana Ngaluko.

HABARI KIMATAIFA

# Spika wa Marekani achana hotuba ya Trump

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, juzi usiku alisoma hotuba yake ya tatu ya hali ya taifa kwa kuelezea hatua ambazo utawala wake umepiga katika kuimarisha uchumi tangu alipoingia madarakani.

Rais Trump alikuwa akilihutubia taifa kwenye majengo ya bunge na kwamba alielezea sera za utawala wake na kusema kwamba alikuwa ametimiza ahadi alizotoa wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2016.

Hata hivyo, punde tu baada ya hotuba hiyo, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Nancy Pelosi, akionekana mwenye hasira, alichana nakala ya hotuba hiyo na kuitupa mezani.

Awali, Rais Trump alishangiliwa na wabunge wa chama cha Republican muda mfupi baada ya kuanza hotuba yake.

Pamoja na kusifia juhudi zake za kuimarisha uchumi, Rais Trump ambaye anakabiliwa na mashtaka ya kuondolewa madarakani alizungumzia masuala mengine kadhaa kama vile sera zake kuhusu elimu, uhamiaji, jeshi la Marekani, ugaidi na nafasi za ajira kwa Wamarekani weusi na wanawake.

Katika tukio lingine la kushtukiza, Rais Trump alimkaribisha kiongozi wa upinzani wa Venezuela, Juan Guaido, ambaye alikuwa ndani ya ukumbi huo wa bunge.

Aidha, Trump aliwatuliza baadhi ya wageni walioalikwa, ikiwa ni pamoja na mtangazaji maarufu wa redio Rush Limbaugh, anayefahamika kwa kutetea sera za Warepublican.

Mwanzoni mwa hotuba hiyo, tukio lisilo la kawaida lilijiri pale Rais Trump alionekana kama alipuuza ishara ya Spika Pelosi, ambaye alikuwa amemnyooshea mkono wa kumkaribisha kwenye jukwaa ili kuanza hotuba yake.

Rais Trump alipita bila kumwangalia Pelosi na kusimama mbele yake tayari kwa hotuba hiyo.

Hotuba hiyo ilijiri wakati Wamarekani wamegawanyika kisiasa kufuatia hatua ya Baraza la Wawakilishi kuwasilisha mashtaka ya kutaka kumwondoa mbele ya baraza la seneti, huku taifa likielekea kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu.

**VOA**

# Moi kuzikwa wiki ijayo nyumbani kwake

**NAIROBI, Kenya**

MWILI wa Rais mstaafu wa Kenya, Daniel Arap Moi, aliyefariki juzi utazikwa nchini humo Jumatano ijayo Februari 12, 2020.

Taarifa iliyotolewa na familia yake Moi jana ilieleza kuwa mazishi hayo yatafanyika nyumbani kwake Kabarak.

Naye Mbunge wa Tiaty, William Kamket ambaye ni mjumbe kamati ya mazishi alisema shughuli ya kuuaga mwili wa Moi utafanyika katika uwanja wa mpira wa Kasarani Jumanne, Februari 11, 2020.

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta alitangaza kifo cha Moi usiku wa kuamkia juzi, Moi amefariki akiwa na umri wa miaka 95 katika Hospitali ya Nairobi alikokuwa anapata matibabu.

Taarifa zinaeleza kuwa Moi alizaliwa Septemba 2, 1924, katika jamii ya wakulima katika eneo la Baringo, Magharibi mwa Kenya.

Jina lake la kwanza lilikuwa Toroiticha Arap (mwana wa) Moi, lakini baadaye akabatizwa katika ukristo na kupewa jina la Daniel wakati huo akiwa mwanafunzi.

Moi alikuwa Rais wa Kenya kuanzia mwaka 1978 hadi 2002, alikuwa mmoja wa mwanasiasa mashuhuri waliofanikiwa, akitoka jamii ndogo ya Tugen, mojawapo ya makundi yanayounganisha kabila kubwa la Wakalenjin.

Alianza kufanya kazi kama mwalimu mwaka 1945 katika Shule ya African Government School na mwaka mmoja baadaye akiwa na umri wa miaka 22 akateuliwa kuwa mwalimu mkuu.

Machi 1957 Moi alikuwa mmoja wa watu weusi nane waliochaguliwa kuwa wanachama wa Bunge la ukoloni lilitwalo LegCo.

***CITIZEN***



Rais wa Marekani, Donald Trump akitoa hotuba yake ya tatu ya hali ya Taifa hilo. **PICHA: REUTERS**

# Kenya kuwarejesha wanafunzi waliopo China

**NAIROBI, Kenya**

KENYA inapanga kuwarudisha nyumbani wanafunzi 85 ambao wamekwama katika mji wa Wuhan nchini China, ambako ndiyo kitovu cha mlipuko wa virusi vya corona.

Hata hivyo, imesema pindi wanafunzi hao watakapowasili Kenya watatengwa ili kupimwa afya zao.

Waziri wa Afya nchini humo, Dk. Mercy Mwangangi, aliyasema hayo jana wakati alipokutana na kamati ya afya ya bunge na kwamba wanafunzi hao watarejeshwa nchini Kenya pindi China itakapoondoa zuio la usafiri katika mji huo.

"Waziri wa Mambo ya Nje anawasiliana mara kwa mara na wanafunzi 85 wa Kenya," alisema Dk. Mwangangi na kuongeza:

"Tumetenga vyumba viwili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta na kutenga chumba cha kufuatilia wagonjwa katika Hospitali ya Kenyatta. Pia vituo zaidi maalumu vimetengwa katika Jimbo la Nairobi," alisema Dk. Mwangangi.

Bado haijafahamika iwapo zuio la usafiri katika mji wa Wuhan litaondolewa lini, lakini nchi kadhaa zimekuwa zikihamisha raia wake walioko kwenye mji huo. Misri ilikuwa nchi ya kwanza kuchukua hatua hiyo.

Shirika la Afya Dunia (WHO) limesema kwamba lina wasiwasi kuhusu namna nchi za Afrika zilivyojitayarisha kukabiliana na virusi hivyo.

Juzi, meneja wa kukabiliana na hali za dharura barani Afrika kutoka (WHO), Dk. Michel Yao, alisema nchi nyingi za Afrika zina mfumo dhaifu wa afya.

Dk. Yao alisema kwamba kuna maabara sita pekee barani Afrika zenye uwezo wa kuchunguza virusi vya corona ambazo ni Nigeria, Ghana, Madagascar, Sierra Leone na Afrika Kusini.

"Afrika Kusini imefanya vipimo 71 vya ugonjwa huo kutoka nchi mbalimbali ambavyo vilikuwa vinashukiwa kuwa ugonjwa wa corona. Hata hivyo vipimo vyote vimeonyesha kwamba virusi hivyo siyo vya corona," alisema Dk. Yao.

WHO limesema kwamba litatoa usaidizi kwa nchi 24 ili ziweze kufanya utafiti wa matukio ya ugonjwa huo ambavyo hadi kufikia sasa vimesababisha vifo vya watu 426 nje ya China.

Hadi kufia sasa Afrika haijathibitisha kisa chochote cha ugonjwa huo.

***BBC***

# Mfanyabiashara adaiwa kuficha wahamiaji haramu nyumbani

Na Idda Mushi, MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limedai kuwakamata watu watano raia wa Somalia wakiwa wamefichwa nyumbani kwa mfanyabiashara, Mpinga Pyuza (30), mkazi wa Mji Mpya katika Manispaa ya Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alidai mbele ya waandishi wa habari jana kuwa watu hao wanaodaiwa wahamiaji haramu, walikamatwa baada ya polisi kupokea taarifa za kiintelijensia kutoka kwa raia wema.

Aliwataja raia hao wa Somalia waliokamatwa kuwa ni Sadack Hassan (20), Hassan Ally (21), Mahmud Mahamad(30), Sadam Ally(21) na Mahamad Ibrahim (30), ambao bado wanaendelea kuhojiwa na ili hatua za kuwafikisha mahakamani kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji zifanyike.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kupata taarifa za uhalifu na kuwafichua wanaojihusisha na biashara zote haramu za kusafirisha binadamu na dawa za kulevya.

Katika tukio lingine, askari waliokuwa doria katika maeneo mbalimbali mkoani Morogoro, wamewatia mbaroni watu 14 wanaodaiwa kuwa ni wauzaji, watumiaji na wasafirishaji wa dawa za kulevya aina ya bangi.

Kamanda Mutafungwa alidai watuhumiwa hao walianza kukamatwa Januari 23 mwaka huu eneo la Mizani Mikese wilayani Morogoro.

Alidai kuwa askari wake walilikamata gari aina ya Toyota Land Cruiser likiendeshwa na Elias Nkurua (30) akiwa na mwenzake Swalehe Ally (32), wakazi wa Mbagala jijini Dar es Salaamu wakiwa wamepakia viroba tisa vya bangi wakitokea Doma wilayani Mvomero kuelekea jijini Dar es Salaam.

Alidai mtuhumiwa mwingine, Plasdus Mandala, alikamatwa Januari 28 majira ya saa saba mchana katika geti la Maliasili lililoko Mkamba wilayani Kilombero akiwa na bangi kilo 9.5 iliyokuwa imehifadhiwa kwenye begi jeusi.

Kamanda Mutafungwa alidai mtuhumiwa alikamatwa akiwa anasafirisha bangi hiyo katika basi aina ya Scania, mali ya Kampuni ya Dar Express lililokuwa likitoka Mahenge kuelekea jijini Dar es Salaam na bangi hiyo ilikuwa imehifadhiwa katika buti la basi hilo.

Wengine waliokamatwa ni Joseph Mbagala (24), mkazi wa Tegeta aliyekamatwa na bangi debe moja iliyokuwa imehifadhiwa ndani ya begi jeusi, Yohana Philipo (15), Issa Hatibu na Kadili Hassan (27) na Omary Pastori (20), wote wakazi wa Chamwino waliokutwa na kete 42 za bangi zilizohifadhiwa kwenye vipande cha gazeti.

Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Juma Kibanike, mkazi wa Kichangani aliyekamatwa na kete 24 alizokuwa amezihifadhi ndani ya chupa ya plastiki, Swamadu Kiswili, mkazi wa Viwanja Sitini, Ifakara, Kilombero aliyekamatwa na bangi kete 11 na Amandusi Zakaria (26), mkulima na mkazi wa Sokoine, aliyedaiwa kukamatwa na bangi viroba viwili akiwa ameanika juani.

Kamanda huyo pia aliwataja watuhumiwa wengine waliokamatwa kuwa ni Robert Andrea, mkulima na mkazi wa Mafinga aliyekamatwa na bangi kete 17 alizohifadhi katika mfuko wa suruali yake, Christina Isaya (41), mkulima na makazi wa Msamvu Ruaha, aliyekamatwa na bangi inayokadiriwa kuwa robo kilo.

Wengine ni Andrea Nafiris (44), mkulima na mkazi wa Msamvu Ruaha, aliyedaiwa kukutwa na kete 34 na Asha Peter (28), mkazi wa Kijiji cha Dumila Magole aliyedaiwa kukamatwa na misokoto 80 nyumbani kwake.




Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, akizungumza na waandishi wa habari wakati akizindua mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu (MAKISATU 2020) mjini Dodoma jana. Mashindano hayo yatamalizika mwezi ujao na yamedhaminiwa na Benki ya CRDB, ambapo itatoa Sh. milioni 50. Wengine ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo na ujumbe wa benki hiyo ulioongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa, Prosper Nambaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka sheria ya udhibiti matumizi mabaya ya noti

Na Dege Masoli, KOROGWE

MWANAHARAKATI wa vita dhidi ya umaskini nchini, Patrick George, ameshauri kuwapo sheria ya kuwakamata na kuwafungulia mashtaka watu wasiyo na nidhamu ya utunzaji wa noti.

Mwanaharakati huyo alisema juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akisema pamoja na mambo mengine, hali halisi ya umaskini inatokana na kutotunza noti.

Patrick alisema asilimia kubwa ya Watanzania hawana nidhamu ya utunzaji wa noti na kwamba katika matumizi yao husababisha fedha hizo kuchakaa kabla ya wakati kutokana na kuziweka katika mazingira machafu yasiyo na nidhamu na thamani yake. Alielezea umuhimu wa kuwapo mjadala juu ya mazoea yaliyojengeka miongoni mwa Watanzania ya kuchafua na kuchakaza noti kabla ya wakati kutokana na kuziweka katika mazingira mabaya.

Kwa mujibu wa Patrick, tabia hiyo inaweza kukomeshwa hatimaye kujenga nidhamu ya fedha nchini.

"Asilimia kubwa ya Watanzania hawatambui thamani ya vitu vyao ikiwamo utunzaji wa fedha. Kwa mfano utamkuta muuza bucha au samaki kakunjakunja noti na kurejesha chenji kwa mteja iliyochafuka kwa damu na harufu ya vumba. Jambo hili ni fedheha kwa taifa kwa raia wa kigeni wanaohudumiwa katika mazingira hayo," alisema.

Hata kama hiyo, hupatikana pia kwa mamalishe ambao hufungafunga noti kwenye kanga, kitendo alichodai licha ya kuziondolea thamani na hadhi fedha hizo.

Pia alisema hali hiyo huzifanya fedha kuchakaa haraka kutokana na kukosa uhifadhi bora na kutaka iwapo sheria ya kuwataka watu kutunza fedha hizo na kuchukuliwa hatua.

Aidha, alipendekeza uwapo wa sheria ya kuwakamata wanaochana noti na pia kuwapo na kipengele cha kuwadhibiti wanaozichafua hatimaye wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma ya kutoheshimu fedha ambazo alidai ni nembo ya taifa.

"Nimefanya uchunguzi na kubaini Watanzania tuna hulka ya kuchafua na kuchakaza noti bila kujali kitendo hicho ni kuitia hasara serikali. Hii ni tofauti na tofauti na nchi za wenzetu ambao watu wake wana nidhamu ya hali ya juu kwenye matumizi na mpaka utunzaji wa noti zao wakitambua kuwa ndiyo nembo ya utaifa wao," alisema.

Mwanaharakati huyo alisema anaamini uchumi wa kuanzia ngazi ya familia hadi taifa unajengwa na mambo mengi, ikiwamo nidhamu ya fedha ambayo inaanzia kwenye matumizi hadi utunzaji wake.

# Walilia elimu uchunaji ngozi

Na Mary Mosha, MOSHI

WAKATI serikali ikijipanga kuingia katika uchumi wa viwanda, wadau wa sekta ya ngozi wameombwa kutoa elimu juu ya uchunaji ngozi ili ziwe na tija kwa wafugaji kwa kuziuza na hatimaye kutumika kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Hiali hiyo inatokana na na baadhi ya wachunaji wa ngozi kutokuwa na elimu ya kutosha, hivyo kusababisha ngozi inayochunwa kuwa na kasoro mbalimbali kama vile matobo na kuifanya ishuke thamani ikilinganishwa na inayotoka nchi jirani

Sabas Woisso, Mkurugenzi wa Kiwanda cha Ngozi cha Himo Tanaries (HITA) alisema juzi kuwa kumekuwapo na changamoto kubwa katika uchakataji wa ngozi huku kasoro zilizoonekana zikichangia kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo kwa kila mwaka.

"Tukiwa katika hatua za kwenda katika uchumi wa viwanda ni lazima kuhakikisha kuwa tunakuwa na malighafi nzuri za kutosha katika viwanda vyetu ili fedha zinazopatikana zimrudie mfugaji moja kwa moja.

"Sasa tunaelekea katika uchumi wa viwanda, hivyo ni lazima tuhakikishe ngozi ambazo tutazitumia katika nchi yetu kuzalisha bidhaa mbalimbali zinakuwa na ubora ili soko letu liwe la kimataifa na kufahamika zaidi ndiyo maana nasema wadau wa sekta ya ngozi huu ndio muda mwafaka wa kujipanga katika hili," alisema Woisso.

Kwa mujibu wa Woisso, bado kuna uelewa mdogo kwa wafugaji juu ya kutunza ngozi ili kuwa na bei katika soko la dunia na kwamba kwa maeneo mengi, wafugaji hawana uelewa wa kutosha juu ya uchunaji pamoja na uhifadhi.

"Ng'ombe unakuta wanapigwa chapa sehemu zisizo maalumu au unaenda machinjioni unamkuta mchunaji kalewa chakari anatoboa toboa ile ngozi bila sababu yoyote ile. Sasa hii inashusha thamani ya ngozi," alisema.

Katika hatua nyingine, Woisso aliiomba serikali kujenga mikakati katika kuinua sekta ya ngozi nchini ikiwamo kuwajengea uwezo juu ya kutengeneza bidhaa za ngozi sambamba na utafutaji wa masoko.

Alisema kinachofanyika hivi sasa kwa watengenezaji wa bidhaa za ngozi ni kujitafutia elimu au kutafuta wataalam nje ya nchi kitu ambacho bado ni gharama kwa wazalishaji hao.

Hata hivyo, Woisso aliishukuru serikali kwajitihada ambazo imeonyesha kwa kusisitiza kununua bidhaa za ndani kwa kuwa kufanya hivyo ni kufanya wajasiriamali wa ndani kukuza mitaji yao tofauti na kuendeleza kuagiza kutoka nje ya nchi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**
Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji
**Apige: SImu Namba:**
**0786 641903 au 0716 172929**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI



**Baraka Barthy** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0867-0053 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari Pandahili

Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/SEL/RB/100527/2020**

115617902

### KUPOTEA KWA CHETI



**Raina Komugisha Syliacus anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0586-0061 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Kaisho.**
**Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote Polisi.**

**Polisi Taarifa: MW/RB/4515/2015**

115617402

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NUURIDIN OMARI KIHIYO**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya
**TOYOTA TOWNACE**
yenye namba za usajili
**T 165 DMW.**
Chassis no. **KM 510028383,**
Egine no. **Z35ICD.**
yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi
**DOD/DOD/RB/113078/2020.**

115617702

### KUPETELEWA KADI YA PIKIPIKI.

NDUGU JANUARI MELKIADES MAZINGO, MKAZI WA KIBWIGWA, WILAYA YA BUHIGWE MKOA WA KIGOMA, ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI T 788 BLQ (DT).

KADI HIYO IMESAJILIWA KWA JINA LA MUSA ITRA BANIGWA.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA AU KUIOKOTA AIPELEKE KITUO CHA POLISI ALICHO NACHO KARIBU.

AU AWASILIANE NA MIMI KWA SIMU NAMBA 0766 709825

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi No; 27/2020

Ombi la GETRUDA SAKURANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAKURANI EUDESI MUSHI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/02/2020.

HAKIMU

115617802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Maria Saimoni Pangalas** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4563/0017** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Makange.

Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote Polisi.

**Polisi Taarifa :**
**DAR/MBU/RB/38501/2020**

115616902

### KUPOTEA KWA CHETI



**Jacqueline Amos** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0283-0006 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari John The Baptist

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote Polisi.

Polisi Taarifa : 10811592527

115617202

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**LAND CASE NO. 20 OF 2019**
**ESTOMII ORONGOI................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**EDWARD MEMIRIEKI AND 24 OTHERS.........DEFENDANT**

**NOTICE OF PRELIMINARY OBJECTION HEARING**

**TO MR.DEO ASSEY**
**C/O**
**MURIET WARD EXCECUTIVE OFFICER**
**P.O.BOX 3113**
**ARUSHA.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Preliminary Objection Hearing in the High Court at Arusha on the 10th day of February,2020 at 08:30 a.m .o'clock in the forenoon.

YOU may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time before hearing the court may proceed in your absence.

GIVEN under my HAND and the SEAL of the COURT this 16th day of January,2020.

**S.P.Mwaiseje**
**DEPUTY REGISTRAR**
**ARUSHA.**

### KUPOTEA KWA KADI

**Rakesh Babu Tulsidas** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya uasajili T687 DHW iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CHA/RB/97387/2020

115617102


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# FERDINAND

## AWAONYA UTD JUU YA GREENWOOD

**MANCHESTER, England**

MANCHSTER United lazima ipunguze kumpa muda zaidi na kuonyesha umuhimu kwa Mason Greenwood mapema hivi katika kipindi chake cha uchezaji, kwa sababu kufanya hivyo kunaweza kusababisha yaliyomkuta Michael Owen, kwa mujibu wa Rio Ferdinand.

Greenwood aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha United msimu uliopita na amecheza mechi tatu, ikiwamo ya kwanza waliyoshinda dhidi ya Cardiff City.

Umuhimu wake kwenye kikosi umeongezeka haraka baada ya kuondoka kwa Romelu Lukaku, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, akicheza mechi 32 kwenye mashindano yote.

Na kuumia kwa hivi karibuni kwa Marcus Rashford kunamaanisha kwamba atakuwa na nafasi zaidi ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza, lakini nahodha wa zamani wa United, Ferdinand haoni kama ni afya kuanza kumpa majukumu makubwa Greenwood mapema hivyo, kwani anahofu atashuka haraka kiwango kama Owen.

Owen mchezaji wa zamani wa Liverpool, Real Madrid na United aling'ara haraka akitokea kwenye Akademi ya Anfield mwanzoni mwa miaka ya 1990 na kuwa nyota mkubwa wakati akiwa bado kinda, na akashinda Ballon d'Or mwaka 2001, lakini baadaye akajikuta akikabiliwa na majeraha ya mara kwa mara na ufiti.

Akizungumza na vyombo vya habari vya England Jumanne, Ferdinand alisema: "Kijana (Greenwood) ni mfungaji mzuri.

"Licha ya kwamba bado mdogo ana uwezo mkubwa wa kufunga mabao kwa urahisi. Lakini kwa sasa anahitaji muda zaidi na si sawa kupewa kipaumbele.

"Unaweza kumtarajia yeye kucheza kila mchezo kwa sababu ya majeruhi ya Marcus na hapo mtamfanya anyanyue mabega juu.

"Mfano mzuri kwa hilo ni kama ilivyokuwa kwa Michael Owen. Alichomoza kama 'kijana wa maajabu', akiwa na matarajio mengi na alicheza mechi nyingi mno akiwa kijana mdogo.

"Nafikiri hiyo ndio ilikuwa sababu kubwa kwake yeye kuwa na majeraha ya mara kwa mara katika maisha yake ya kisoka na ikamfanya ashuke kiwango chake haraka na ndivyo inavyoweza kutokea kwa Greenwood."

# POGBA AFUNGUKA TENA KUONDOKA MAN UNITED

**Manchester, England**

Paul Pogba amewaambia wachezaji wenzake wa Manchester United, bado anahitaji kuondoka klabuni hapo majira ya joto.

Pogba, 26, ameanza mechi sita tu msimu huu kutokana na kuumia kifundo cha mguu katika vipindi viwili tofauti na bado anatamani kuhitimisha nyakati zake hapo United, huku Real Madrid na Juventus zikiendelea kuvutiwa na huduma yake.

Chanzo kimoja kutoka ndani ya kikosi cha United kililiambia MEN kuwa akili ya Pogba kwa sasa 'haipo klabuni hapo' na wachezaji wengi wanaamini anaendelea kuwapo kwa ajili ya maslahi ya klabu. Pogba bado anabaki kuwa mtu maarufu sana kati ya marafiki na wachezaji wenzake, ambao wanaelewa msimamo wake.

Pogba alieleza matamanio yake ya "changamoto mpya' Juni mwaka jana pamoja na wakala wake, Mino Raiola alidai 'yupo katika mchakato' wa kushughulikia uhamisho ambao haukukamilika. Na zaidi hivi karibuni, Raiola alisema 'samahani' hawezi kumpeleka Pogba Madrid na kwamba hawezi 'kumleta yeyote yule' United.

United ilimthaminisha Pogba na takriban pauni milioni 180 majira ya joto yaliyopita, lakini kiufundi sasa anaingia miezi 18 ya mwisho katika mkataba wake.

Hata hivyo, United ina nafasi ya kumwongeza mwaka mmoja zaidi wa kumfunga Pogba klabuni hapo hadi mwaka 2022, lakini kutokana na umri wa dili hilo pamoja na matatizo yake ya kifundo cha mguu, yanasababisha thamani ya Mfaransa huyo kupungua.

Pogba alirejea dimbani akitokea kuuguza majeraha yake kwa kipindi cha miezi mitatu na kucheza kwa dakika 71 dhidi ya Watford Desemba 22, mwaka jana kabla ya kufanyiwa mabadiliko 'sab' katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Vicarage Road na kisha alicheza dhidi ya Newcastle United Siku ya Kufungua Zawadi [Boxing Day'] kabla ya kuhitaji kufanyiwa upasuaji.



# Gervinho apewa adhabu Parma



**ROME, Italia**

KLABU ya Parma imemwamuru Gervinho kufanya mazoezi peke yake hadi hatua nyingine itakapochukuliwa dhidi yake baada ya kushindwa kukamilisha uhamisho alioulazimisha wa kwenda Al Sadd.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal aliamua kutohudhuria mazoezi wiki iliyopita ili kulazimisha uhamisho wake wa kwenda klabu hiyo inayonolewa na Xavi kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni tano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alionekana kukaribia kukamilisha uhamisho huo, lakini ulishindwa kufanikiwa kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha dogo la usajili Januari 31.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, sasa atalazimika kubakia hapo Parma kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki, lakini anakabiliwa na wakati mgumu kwa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

Taarifa ya klabu iliyotolewa Jumanne ilisema: "Baada ya kukosekana kwenye mazoezi bila sababu yoyote wiki iliyopita, Parma inaweza kuthibitisha kwamba, Gervinho atafanya mazoezi peke yake chini ya maelekezo ya benchi la ufundi la klabu hadi hatua zaidi zitakapotangazwa."

Gervinho amecheza mechi 17 za Ligi Kuu msimu huu, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho tatu.

Parma, ambao watacheza na Lazio Jumapili, wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya mechi 22.

## ROONEY KUIVAA MAN UNITED KOMBE LA FA

**LONDON, England**

PHILLIP Cocu amesema Wayne Rooney atakuwa tayari kucheza dhidi ya klabu yake ya zamani ya Manchester United baada ya Derby County kufuzu kucheza kwenye Kombe la FA raundi inayofuata dhidi ya miamba hao wa Ligi Kuu ya England.

Nahodha huyo wa Derby na nahodha wa zamani wa United, Rooney mwenye umri wa miaka 34, alifunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 77 na wakati wakiwafunga Northampton Town 4-2 kwenye mchezo wa marudiano wa raundi ya nne wa Kombe la FA.

Rooney, ambaye aliondoka United mwaka 2017 na kuwasili pale Everton mwaka 2004, sasa atakabiliana na United, ambako aliweka rekodi ya kuwa mfungaji bora aliyewafungia 'Mashetani Wekundu' hao mabao 253.

Pale Derby akiwa kocha mchezaji tangu Januari baada ya kucheza kwa misimu miwili kwenye Ligi Kuu ya Marekani akiwa na DC United, na sasa Rooney yupo tayari kwa mchezo huo wa Kombe la FA, kwa mujibu wa kocha mkuu wa timu hiyo, Mholanzi Cocu.

"Alikuja kutoka Marekani, alijiunga na sisi na sasa atacheza dhidi ya klabu yake ya zamani... ni kitu cha kuvutia kwake, nina uhakika atakuwa tayari," alisema Cocu akiwaambia waandishi wa habari.

"Utakuwa mchezo mzuri si tu kwa Wayne, lakini kwa kila mtu klabuni hapa."

Mchezo huo wa Derby dhidi ya United utachezwa kati ya Machi 3 na 5, huku ukiwa hauna kurudiana.



## BOBAN AMCHAMBUA IBRAHIMOVIC MILAN

**MILAN, Italia**

MILAN daima itamshukuru Zlatan Ibrahimovic kwani "hakuwa na cha kuthibitisha kuhusu ubora wake" na "chochote cha kupoteza" kwa kurudi kwake kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Soka, Zvonimir Boban.

Ibrahimovic alijiunga tena na Milan mwezi uliopita baada ya kuondoka pale Rossoneri mwaka 2012, na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 38, umuhimu wake umeonekana haraka hapo kwenye dimba la San Siro.

Tangu alipowasili hapo kwa uhamisho huru kutoka Ligi Kuu ya Marekani (MLS), pale katika klabu ya LA Galaxy, Ibrahimovic ameongeza morali kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na amefuga mara mbili katika mechi tano alizocheza.

Milan haijapoteza tangu Ibrahimovic alivyorudi katika mechi saba na Boban amemsifia nyota huyo wa zamani wa Manchester United na Paris Saint-Germain.

"Ibra ni mchezaji anayevutia na mwenye kiwango bora kabisa," alisema Boban, ambaye timu yake ya Milan ipo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Serie A.

"Alijiunga na timu kwa hali ya unyenyekevu mkubwa licha ya kuwa yeye ni mchezaji mkubwa anayeheshimika na timu nyingi duniani.

"Ameonyesha umuhimu wake kwa wachezaji wenzake vijana na kuja kwake kumeongeza ari na kujiamini kwa wachezaji.

"Haikuwa rahisi, lakini alifahamu namna gani wachezaji walivyokuwa kwa wakati huo na yeye ameweza kuielewa hali hiyo haraka sana."



# KANE

## DIMBANI SASA HADI MEI - MOURINHO

**LONDON, England**

JOSE Mourinho anaamini Harry Kane hataweza kurudi uwanjani kuichezea Tottenham angalau hadi Mei mwaka huu, hilo likiwa pigo kubwa kwa klabu na nchi yake.

Mshambuliaji huyo wa Spurs, Kane aliumia misuli kwenye mchezo wa mwaka mpya wa kichapo kutoka kwa Southampton na amekuwa nje ya uwanja tangu hapo, akiwa amefanyiwa upasuaji.

Awali ilitarajiwa Kane angekuwa nje ya dimba hadi Aprili na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, tayari ameanza mazoezi ya taratibu ya viungo.

Hata hivyo, Mourinho ameonyesha shaka akibainisha kwamba hamtarajii nahodha huyo wa England kuwa tayari kucheza hadi Mei 9 hadi 10, huku Spurs ikicheza dhidi ya Leicester City na Crystal Palace kwenye mechi zake mbili za mwisho za msimu huu wa Ligi ya England unaofikia tamati Mei 17.

"Mechi dhidi ya Leicester," alisema Mourinho, ambaye kikosi chake jana Jumatano kilikuwa kinacheza na Southampton kwenye mchezo wa marudiano wa Kombe la FA.

"Pengine tunahitaji mchezo huo kwa kitu fulani. Kuwa wa nne, kuwa wa tano au wa sita. Pengine anaweza kutusaidia kwenye mchezo huo. Natumaini."

Kama matarajio hayo ya Mourinho yatakuwa sawa, inamaanisha Kane atakuwa tayari kucheza mechi mbili tu zilizobaki kwenye Ligi Kuu na kuelekea kujiunga na kikosi cha England cha kocha, Gareth Southgate kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

England watacheza mechi za kujipima nguvu Juni mwanzoni dhidi ya Austria na Romania - kabla ya kuwavaa Croatia kwenye mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020 Juni 14.

Suala la timu ya taifa si kubwa sana, kwani Kane anaweza kuwa fiti kwa ajili ya michuano hiyo, kwa mujibu wa Mourinho.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ALIAMSHA BARCA AKIMSHUKIA ABIDAL

Nafikiri wakati unapowazungumzia wachezaji, unatakiwa kuwataja majina, kwa sababu...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amemjia juu Mkurugenzi wa Soka wa Barcelona, Eric Abidal, ambaye alibainisha kwamba baadhi ya wachezaji walikuwa hawajitumi vya kutosha na kusababisha kutimuliwa kwa Ernesto Valverde.

Abidal alifanya mahojiano na vyombo vya habari vya Hispania Jumanne na Mfaransa huyo aliezea sababu kadhaa za kutimuliwa kwa Valverde Januari.

Alibainisha kwamba, walianza kufikiria kubadilisha kocha baada ya mchezo wa Clasico wa sare ya bila kufungana na Real Madrid Desemba 18, mwaka jana huku beki huyo wa kushoto wa zamani akidai yeye na stafu wenzake waligundua "wachezaji wengi walikuwa hawajitumia na kulikuwa na tatizo la mawasiliano ya ndani."

Lakini Messi, ambaye mara chache sana hujiingiza kwenye mgogoro wa klabu, amemjia juu Abidal na kumwambia anatakiwa kuwataja majina wachezaji hao badala ya kuwahusisha wote kwenye "upuuzi" huo.

Akiandika kwenye ukurasa wake wa Instagram akinukuu tuhuma hizo za Abidal, Messi alisema: "Kwa ukweli kabisa sipendi kufanya vitu hivi, lakini kila mmoja anatakiwa kuwajibika na majukumu yake na kuchukua hatua.

"Wachezaji (wanaohusika) kwa kile kinachotokea uwanjani na sisi pia tunakuwa wa kwanza kutambua wakati ambao hatuchezi vizuri.

"Majukumu hayo yako kwenye eneo la utawala wa michezo na wao wanatakiwa kutekeleza majukumu yao hasa kwa maamuzi wanayoyafanya.

"Mwisho, nafikiri wakati unapowazungumzia wachezaji, unatakiwa kuwataja majina, kwa sababu bila ya hivyo inaonekana wote tunahusika wakati si jambo la kweli."

Barca watashuka tena dimbani leo, Alhamisi kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la Mfalme [Copa del Rey] dhidi ya Athletic Bilbao.

## KWA UFUPI

**JUVE NAYO KWA SANE**
Juventus inazingatia suala la kwenda kumsajili winga wa Manchester City na Ujerumani, Leroy Sane, 24, katika majira ya joto, wakati huu Mjerumani huyo akiwindwa pia na Bayern Munich. ***(Calcio Mercato, via Inside Futbol)***

**LAMPARD NA FUNGU SOKONI**
Chelsea inajiandaa kumpa kocha Frank Lampard pauni milioni 150 kwa ajili ya usajili wa majira ya joto huku mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 23, akiwa ndiye anayemmulika zaidi. ***(Evening Standard)***

**STONES NJIA PANDA CITY**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka kusajili mabeki wa kati wawili katika majira ya joto, usajili ambao unauweka mashakani mustakabali wa baadaye wa beki wa England, John Stones, 25. ***(Times)***

**GREALISH SASA LULU UNITED**
Manchester United itatoa kipaumbele kwa kwenda kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, 24, katika majira ya joto wakati huu Muingereza mwenzake James Maddison, 23, akikaribia kusaini mkataba na Leicester City. ***(Mirror)***

**POCHETTINO AMULIKWA ATLETICO**
Atletico Madrid inafuatilia upatikanaji wa kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino endapo wataachana na Diego Simeone majira ya joto. ***(Telegraph)***

**KOKCU AIVUTIA ARSENAL**
Arsenal inavutiwa na kiungo wa Feyenoord na Uturuki U-21, Orkun Kokcu, 19. ***(Mail)***

**BENRAHMA ATETWA NEWCASTLE**
Leicester City na Newcastle United zinajiandaa kulipa pauni milioni 15 kwa winga wa Brentford na Algeria, Said Benrahma, 24, katika majira ya joto. ***(Sun)***

**WAKALA WA BALE AIKANA SPURS**
WAKALA wa Gareth Bale, amekanusha taarifa kuwa Tottenham ilitoa ofa kwa mshambuliaji huyo wa Real Madrid na Wales wakati wa dirisha la Januari. ***(Talksport)***

**ATHLETIC YASIKILIZIA KWA KEPA**
Athletic Bilbao imeelekeza macho yake kwa kipa wao wa zamani, Kepa Arrizabalaga, 25, baada ya Mhispania huyo kutopewa nafasi na kocha wa Chelsea, Frank Lampard katika mechi dhidi ya Leicester City. ***(Sun)***

**HODGSON AIFUNGUKIA PALACE**
KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, 72, anaweza kuondoka katika dimba la Selhurst Park majira ya joto kama hatahakikishiwa mipango ya usajili kuelekea dirisha la majira ya joto. ***(Times)***

**ROMERO ANUKIA KUSEPA UTD**
Manchester United inatarajia kipa wao, Muargentina Sergio Romero, 32, kuondoka majira ya joto, pamoja na mlinda mlango namba tatu, Muingereza Lee Grant, 37. ***(Sun)***



HABARI MICHEZO

# KOCHA WA POLISI TANZANIA AELEZA SIMBA ILIPOWASHIKA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema wachezaji wake wamekosa uzoefu na ndio sababu ya kuruhusu bao la 'jioni' lililowapa ushindi mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba.

Vinara hao wa Ligi Kuu Bara, Simba walitoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Hamsini alisema walipambana kwa muda mrefu, lakini kosa moja walilofanya dakika za majeruhi, liliwaumiza na kuwapa pointi tatu wapinzani wao.

"Nawapa pongezi wachezaji wangu wameonyesha kile ambacho niliwaambia wafanye na walijitahidi kwa kweli. Kilichotushinda ni uzoefu, wachezaji wengine hawana uzoefu ukilinganisha na wenzao wa Simba, bado timu inajijenga taratibu na kuendelea kutafuta matokeo mazuri," alisema Hamsini.

Nahodha wa timu hiyo, Iddi Mobby, alisema walicheza vema zaidi katika kipindi cha kwanza, lakini waliporejea kumalizia mchezo huo, kikosi chao kilishindwa kuhimili kasi ya Simba kutokana na wachezaji wake kuwa bora zaidi.

"Matokeo tuliyoyapata hatukutegemea, tuliingia na mpango wa kushinda, Simba ubora wao uko katikati, ukishindwa kuwamiliki, basi watakufungeni, sisi tulijaribu kuwazuia kati lakini tulipoteza umakini katika dakika za mwisho, wakatuadhibu, kiukweli uwezo wanao," Mobby alisema.

Aliongeza kuwa mpira ni mchezo wa makosa, hivyo wamekubali matokeo na wanakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata.

"Mpira ni mchezo wa makosa, unapocheza na timu kubwa hutakiwi kuwapa nafasi, wametuadhibu, sisi tulitengeneza nafasi nyingi, lakini straika wetu wameshindwa kuzitumia, Simba wametengeneza nafasi chache, kutokana na ukongwe na uwezo walionao wamezitumia," Mobby alisema.

Polisi Tanzania ambayo imecheza mechi 19 ina pointi 30 na katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ipo kwenye nafasi ya saba huku mchezo wake unaofuata utachezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya wenyeji Coastal Union.

## John Bocco ataka kasi mzunguko wa pili

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, John Bocco, amesema ushindi wa mabao 2-1 walioupata juzi dhidi ya Polisi Tanzania umewapa ari ya kuanza kwa kasi mzunguko wa pili.

Simba juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi huo kufuatia bao la Bocco na lile la dakika ya mwisho la Ibrahim Ajibu.

Akizungumza na gazeti hili, alisema ligi ni ngumu huku kila timu ikiwa inapambana, lakini ushindi huo utawafanya waanze kwa kasi michezo yao ya mzunguko wa pili.

"Tunashukuru kwa ushindi dhidi ya Polisi, umetufanya kumaliza mzunguko wa kwanza kwa ushindi... kiukweli ligi ni ngumu hivyo lazima tupambane kweli kuweza kupata ushindi," alisema Bocco.

Alisema wanajipanga sasa kwa mchezo wao unaofuata ambao utakuwa wa kwanza kwenye raundi ya pili ya ligi msimu huu.

Simba kesho itakuwa mwenyeji wa JKT Tanzania katika mechi ya ligi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Taifa majira ya saa moja usiku kabla ya Jumanne kuvaana na Mtibwa Sugar kwenye mchezo utakaochezwa Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

BAO LA USIKU...



Wachezaji wa Simba wakishangilia baada ya Ibrahim Ajibu kuifungia bao la kuongoza katika dakika za majeruhi ['bao la usiku'] wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens yaua, Yanga Princess kilio

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba Queens imeendelea kufanya vizuri baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji Tanzanite Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara iliyochezwa juzi jijini Arusha wakati watani zao, Yanga Princess wakiangukia pua kwa mabao 2-1 dhidi ya TSC Queens katika Uwanja wa Gwambina, Mwanza.

Simba Queens ilikwenda mapumziko ikiwa mbele kwa bao hilo pekee katika mchezo huo lililofungwa na Opa Clement na kuifanya timu hiyo inayofundishwa na Mussa Hassan ' Mgosi' kufikisha pointi 17.

**Alliance Girls ya jijini Mwanza nayo imeendelea kujiimarisha kileleni baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya mabingwa watetezi, JKT Queens katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba. Kwa matokeo hayo, Alliance Queens sasa imefikisha pointi 22 baada ya kushuka dimbani mara nane.**

Ruvuma Queens ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, imeendelea kutoa dozi kwa kuifunga Kigoma Sisterz bao 1-0 huku Baobab Queens ikiwachapa Mlandizi Queens 2-0 mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, inatarajiwa kuendelea kesho kwa TSC Queens kuwakaribisha JKT Queens, Alliance Girls dhidi ya Yanga Princess, Baobab Queens watavaana na Simba Queens, Tanzanite SC watawakabili Mlandizi Queens, Ruvuma Queens watawafuata Marsh Queens na Kigoma Sisterz itawaalika Panama Queens.

# Ndanda yatamba kutoshuka daraja

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana ilitarajia kuwakaribisha Mbao FC kutoka jijini Mwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Msaidizi wa Ndanda FC, Wilbert Mweta, amesema kikosi chao 'kimeamka' na kimejipanga kufanya vizuri ili kisiteremke daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mweta, alisema kikosi chake kimeimarika na wachezaji wote wako tayari kupambana kuhakikisha hawapotezi pointi kwenye uwanja wa nyumbani.

**Mweta alisema nidhamu ya wachezaji wao imebadilika ukilinganisha na walivyokuwa katika mzunguko wa kwanza na hali hiyo inachangia kucheza katika kiwango cha juu.**


"Tumedhamiria kufanya vizuri katika kila mechi iliyoko mbele yetu, tutapambana na tunaamini tuna uwezo wa kupata matokeo mazuri, kila timu unayokutana nayo ni ngumu, lakini hatutakata tamaa, bado tuko vitani," alisema Mweta.

Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Mtwara (MTWAREFA), Baraka Jamal, aliliambia gazeti hili kuwa wameanza kampeni ya kuhamasisha mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kuishangilia Ndanda FC katika mechi zake zote za nyumbani. Jamal alisema uamuzi huu utasaidia kuongeza chachu ya kupambana na hatimaye kuibakisha timu yao kwenye Ligi Kuu.

Michezo

Alhamisi Februari 6, 2020

Nipashe



Messi aliamsha Barca akimshukia Abidal HABARI UK 30

WAMETAKATA...



Yosso wa Liverpool, Neco Williams na Adam Lewis wakishangilia baada ya timu yao kupata bao pekee dakika ya 75, kupitia kwa beki wa zamani wa Manchester United, Ro-Shaun Williams aliyejifunga na kuifanya Shrewsbury Town kulala kwa bao 1-0 kwenye mechi ya marudiano ya raundi ya nne ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi, baada ya ile ya Januari 26 katika dimba la Montgomery Waters Meadow kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. Liverpool sasa itakutana na Chelsea raundi ya tano. **PICHA: MTANDAO**

# TFF YAWAKALIA MAREFA KITAKO

●●● Yaitisha kikao cha dharura baada ya kukerwa na waamuzi kukubali rundo la mabao yakuotea, sasa...

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya wadau wa soka nchini kuendelea kulalamikia kuhusu maamuzi mbalimbali yanayofanywa na waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoingia hatua ya lala salama, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeitisha kikao cha dharura ili kujadili suala hilo, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya TFF, Salum Chama, alisema shirikisho limeamua kuitisha kikao hicho ili kupata 'dawa' ya kumaliza tatizo hilo ambalo linaonekana kukomaa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Chama, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya TFF, alisema kikao hicho kinatarajiwa kuhusisha kamati yake pamoja na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Wilfred Kidao na wanaamini baada ya majadiliano, watapata ufumbuzi.

"Kesho (leo) saa 8:00 mchana kutakuwa na kikao cha dharura katika ofisi ya Katibu Mkuu (Kidao), mambo yote yatajadiliwa hapo, kwa leo (jana), naomba nisiseme chochote," Chama alisema kwa kifupi alipotakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko yanayoendelea kuhusu waamuzi.

Malalamiko ya waamuzi yamekua sehemu ya majadiliano kwa wadau wa soka zaidi baada ya mwamuzi msaidizi namba mbili kutoonyesha ishara ya kuotea wakati mabingwa watetezi, Simba walipofunga bao la kusawazisha katika mechi dhidi ya Polisi Tanzania iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

"Nyie mnalalamika na kusema kwa mnayoyaona yanayotokea katika mechi zinazohusisha Simba, Yanga na Azam, lakini tunapokutana sisi timu ndogo ndogo, huko mambo ndiyo mabaya zaidi, ni lazima kuwapo na mkakati wa kumaliza tatizo hili haraka," alisema Ally Kamwe, mmoja wa wachambuzi wa soka nchini.

Wakati baadhi ya wadau wa soka wakidai viwango vya waamuzi wa hapa nchini ni vidogo na wengine wanasema makosa wanayofanya yanaviashiria vya kupendelea baadhi ya timu.

"Kama ni makosa ya kibinadamu, kwa nini haya yawe yanatokea kwa timu kubwa tu? Tujitathmini, tukiendelea hivi, tutaendelea kukosa waamuzi katika mashindano mbalimbali yanayoandaliwa na CAF (Shirikisho la Soka Afrika)," alisema mdau mwingine wa soka wa hapa nchini jina tunalihifadhi.

Katika kuhakikisha waamuzi wanakuwa makini na kufuata sheria 17 za mchezo huo kikamilifu, TFF imekuwa ikitoa adhabu za kuwafungia au kuwasimamisha baadhi ya waamuzi wanaobainika kuchezesha chini ya kiwango.

Bingwa wa Ligi Kuu ndio hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati mfalme wa Kombe la FA huelekea kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Mabadiliko Yanga mfumo wa Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kuendana na ushindani, uongozi wa Yanga ya jijini Dar es Salaam, umesema umejipanga kufanya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa klabu hiyo kisasa.

Akizungumza jana jijini, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hersi Said, alisema ili kufikia malengo, GSM ambao ni wadhamini wa klabu hiyo wameamua kuhakikisha wanakamilisha mchakato huo wa mabadiliko kwa kutumia mifano ya klabu za Ulaya zilizoendelea.

"Klabu ya Yanga ilitangaza kamati ambayo itasimamia na kuiongoza klabu kuelekea mfumo wa kisasa na sisi kama GSM pamoja na kuwa na mipango mingi ya kusaidia timu, mbali na kuwekeza katika upande wa benchi la ufundi na wachezaji tunalibeba na jukumu hilo," alisema Said.

Alisema baada ya kuona wajumbe walioteuliwa kufanikisha mchakato huo kubanwa na majukumu yao binafsi, wadhamini wao waliamua 'kupiga hatua' kwa kumleta mtaalamu huyo asaidie kutoa elimu ya mfumo huo mpya unavyotakiwa kufikiwa.

"Tukizungumzia kambi ambayo timu inakaa na uwanja wa kufanyia mazoezi, GSM inasimamia kwa asilimia 100, tukaona haitoshi kuona timu ya Yanga inafanya vizuri uwanjani, tukaona tuwasaidie kuwapeleka katika mfumo ambao klabu itakuwa imara," Said alisema.

"Watu wengi wanaweza wakadhani GSM ina nia ya kuichukua Yanga, ama kuimiliki... hapana sisi lengo letu ni kuisaidia Yanga SC."

Alimtaja Antonio Pinto ambaye aliwahi kufanya kazi katika klabu ya Benfica ya Ureno, atawapeleka kule wanapotaka kwenda na tayari wameingia mkataba wa kutekeleza malengo ya Yanga.

Alisema wanatarajia kufanya mabadiliko kwa kutumia njia sahihi na za weledi huku wakipanga kumpa Pinto kuhakikisha anafikia malengo na vile vile wakiwa karibu na timu yao pamoja na kamati ya mabadiliko ya klabu ili kuhakikisha mabadiliko yatakayofikiwa yanaendana na matakwa halisi ya nchi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >